


# HAKIKA YA AHMADIYYA

*Watu wengi hawathamini ukweli. Hata hawashuhguliki kwa kuupeleleza wenyewe. Hata hivyo ukweli, hususa unohusika na Dini, ni muhimu sana kwa kila mwanadamu kwa ajili ya wokovu wake. Hi hapa ni nafasi nzuri ya kupeleleza na kuelewa ukweli juu Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya - ndiyo Jumuiya ya pekee duniani iliyo na mpango maalum kwa kuufanya Uislamu ushinde dini zote. Ikiwa kweli unapenda Dini ya Kiislamu huna budi kukisoma kitabu hiki HAKIKA YA AHMADIYYA na kufuata mpango huo. Fuata haki. Usitegemee uvumi.*

**Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Tanzania**



HAZRAT MIRZA BASHIRUDDIN  
MAHMOOD AHMAD KHALIFATUL MASIH II

Makala haya yaliandikwa na Khalifa wetu Mtakatifu, Seyidna Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmood Ahmad, Mungu awe radhi naye kwa ajili ya mkutano uliokuwa katika mji wa Sialkot, Bara Pakistan na yakasomwa mbele ya watu wengi siku ya tarehe 31 Oktoba, 1948

Makala haya yaliandikwa katika lugha ya Kiurdu na yakapigwa chapa katika Gazeti linalotoka kila siku liitwalo Alfadhl, Lahore. Tumeona makala haya ni ya maana sana, tena yanaondoa wasiwasi, upinzani na masingizio yote yanayopatikana siku hizi juu ya Ahmadiyya katika mioyo ya watu mbalimbali.

Kwahiyo tumeyafasiri toka Kiurdu na kuyatia katika lugha ya Kiswahili iliyo lugha kubwa ya watu wa Afrika ya Mashariki. Tuna yakini watu wa sehemu hii ya Afrika ya Mashariki kama watasoma kwa fikira na utulivu, makosa mengi yanayoletwa juu ya Ahmadiyya yataondoka katika mioyo yao, na watatambua ukweli wa Ahmadiyya, na wataona furaha kuungana na Waislamu Waahmadiyya ili sisi sote tufanye kazi kwa umoja na kwa taratibu maalumu ya kueneza dini ya Islam katika bara hili. Naomba Mwenyezi Mungu awasaidieni mpate nafasi ya kuyasoma maneno haya kwa busara kubwa, mnusurike kwa kukubali kweli ya Uhamadiyya. Mungu awe radhi nanyi nasi pia. *Waakheru da`wana anil hamdu lillahi rabbil alamin.*

Wassalaam,  
SHEIKH MUBARAK AHMAD H.A.

***Hakika ya Ahmadiyya***

*Kimetungwa na:* Hazrat Mirza Bashir-Ud-Din Mahmood Ahmad r.a.

© Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Tanzania.

Chapa ya mara ya kwanza 1957 nakili 2,000

Chapa ya mara ya pili 1966 nakili 3,000

Chapa ya mara ya tatu 1981 nakili 5,000

Chapa ya mara ya Nne Machi 2000 nakili 5,000

Kimeenezwa na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya

P. O. Box 376

Dar us Salaam

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press,

P. O. Box 376,

Simu; 110473,

Dar us Salaam.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

## AHMADIYYA NI NINI

Ahmadiyya ni nini, na kwa haja gani imesimamishwa? Ndilo swali moja linalotoka mara kwa mara katika roho za watu waijuao na wasiojua. Wajuao wanakuwa na habari zaidi lakini wasiojua wanakuwa na maswali mengi yanayokuwa ya juu juu. Kwa sababu ya kutojua, mambo mengi wanayatunga kwa mawazo yao tu. Mimi, kwanza, kwa kuwafahamisha watu wa namna hii napenda kusema maneno machache - watu ambao, kwa sababu ya kutofahamu, wamezama katika dhana mbaya za namna mbalimbali juu ya Ahmadiyya.

### ISLAM PEKE YAKE INA KALIMAH.

Katika hawa wasiojua wako baadhi ya watu wanaofikiri kuwa Waahmadiyya hawaiamini *kalimah* ya *La ilaha illallahu Muhammad Rasulullah*, na ya kuwa Ahmadiyya ni dini mpya. Hao watu wengine au akili zao zinaanza kufahamu ya kwamba Ahmadiyya ni dini nyingine na kila dini inakuwa na *kalimah* yake basi pia wanafahamu ya kuwa Ahmadiyya ina *kalimah* mpya. Lakini hakika hasa ni hii ya kuwa Ahmadiyya siyo dini mpya wala haina haja kwa dini yoyote iwe na *kalimah*. Bali, zaidi ya hayo, mimi nasema, *kalimah* si alama ya madhehebu au dini yoyote isipokuwa dini ya Kiislam tu. Yaani, kwa kuwa dini ya Kiislam imetukuka zaidi kwa shauri la utakatifu wa kitabu chake, na kwa shauri la nabii wake kutumwa kwa walimwengu wote, na kwa kuwa ni dini inayoweza kuwafaa walimwengu wote, hivyo, Islam imeheshimiwa kwa shauri la *kalimah* yake pia. Dini zingine zina vitabu, lakini maneno ya Mwenyezi Mungu, yaliyotamkwa na Mwenyezi Mungu mwenyewe neno kwa neno, hayapatikani isipokuwa kwa Waislamu. Lakini kwa kusema kitabu fulani ni cha Mumgu, siyo maana yake kuwa kila neno lililomo katika maelezo yanayoelezwa kitabuni humo limetoka kwa Mwenyezi Mungu. Lakini kitabu cha Islam, Qur'an, kimeitwa kwa neno la Kalamullah - Neno la Mungu, yaani kila neno lake limesemwa na Mwenyezi Mungu madhumuni yake.

## **MANENO YA QUR`AN YALITAMKWA NA MUNGU.**

Kitabu cha Musa kilikuwa na madhumuni yale yale yaliyosemwa na Mwenyezi Mungu. Mafundisho ya Isa a.s. aliyokuwa anawaambia watuyalikuwa yale yale aliyopewa na Mungu. Lakini Kitabu cha Musa na mafundisho ya Isa hayakuwa katika matamko yale aliyoyatumia Mwenyezi Mungu. Bila shaka msomaji wa Taurati na Injili na Qur`an kama vile kwa kuweka rohoni mwake jambo hili baada ya kusoma kwa dakika kumi atakata hukumu mara moja ya kuwa Taurati na Injili ijapokuwa madhumuni yao yalikuwa ya Mwenyezi Mungu, lakini matamko yaliyotumiwa yalikuwa si ya Mwenyezi Mungu. Na pia yeye hataona njia isipokuwa kusema ya kuwa Qur`an ndicho kitabu ambacho madhumuni yake yalielezwa na Mwenyezi Mungu na pia matamko yake yalishuka kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Au mnaweza kusema, mtu asiyeamini Qur`an wala Taurati wala haiamini Injili, baada ya kuvisoma kwa dakika chache atakiri kuwa ingawa watu wanaoishikilia Taurati na Injili wanatangaza ya kuwa vitabu hivi viwili vimetoka kwa Mwenyezi Mungu, lakini hawasemi ya kuwa kila neno katika vitabu hivyo limetamkwa na Mwenyezi Mungu. Bali kwa Qura`ani hana budi atasema ya kuwa aliyeleta kitabu hiki anadai ya kuwa madhumuni ya kitabu hiki yametoka kwa Mwenyezi Mungu na kuwa kila neno lililotumiwa kitabuni humo limetoka kwa Mwenyezi Mungu.

Hii ndiyo sababu Qur`an imejiita *Kitabullah* - kitabu cha Mwenyezi Mungu na pia kimejiita *Kalamullah* - maneno ya Mwenyezi Mungu. Lakini Taurati na Injili havikujiita *Kalamullah* wala Qur`ani haikuviita *Kalamullah*. Basi Uislam umetukuka kuliko dini zingine katika jambo hili ya kuwa vitabu vya dini zingine vinaweza kuwa vitabu vya Mungu, lakini siyo maneno ya Mwenyezi Mungu ya kuwa kila neno lililomo humo lilisemwa naye. Lakini kitabu kitakatifu cha Waislamu siyo tu ni kitabu cha Mungu, bali pia ni maneno ya Mwenyezi Mungu, bali pia ni maneno ya Mwenyezi Mungu mwenyewe.

## **FADHILA YA UISLAMU JUU YA DINI ZINGINE**

Hivyo, dini zote zimeanzishwa na manabii, lakini hakuna dini yoyote iliyoleta nabii ambaye ameeleza hekima za mambo yote ya dini na aliyekuwa mfano kamili katika mwendo wake mwema kwa wanadamu

wote. Ukristo ambao ni dini ya juzi juzi umemfahamu Yesu Kristo kuwa mwana wa Mungu, hapo mwanadamu anawezaje kufuata hatua zake maana mwanadamu hawezi kuwa sawa na Mungu. Wala Taurati na Injili havidai ya kuwa nabii Isa a.s. na Musa (alahimu-ssalaamu) walilazimishwa kazi ya kueleza hekima za mambo ya kidini. Lakini Qur`an Tukufu juu ya Mtume Muhammad s.a.w. inasema: *Yuallimukumul kitaaba wal hikmata* (Baqara, fungu la 18), yaani, Nabii huyu anawaambieni amri za Mwenyezi Mungu na hekima zake. Basi Islam kwa hakika imetukuka katika jambo hili pia ya kuwa nabii wake ni mfano mwema kwa dunia nzima. Na haiwafanyi watu wafuate amri zake kwa nguvu, bali inapotoa amri basi kwa kuimarisha imani ya wafuasi wake na kwa kutia shauku katika mioyo yao inawaambia amri zake zina faida kwa kaumu na kwa watu na kwa walimwengu wote.

Hivyo dini ya Kiislam imetukuka kuliko dini zingine kwa sababu ya mafundisho yake. Mafundisho ya Kiislam kwa ajili ya wadogo na wakubwa, maskini na tajiri, mwanamke na mwanamume, wa Mashariki na wa Magharibi, mnyonge na mwenye nguvu, mfalme na raia, bwana na mtumishi, mume na mke, mama na baba na watoto, anunuaye na auzaye, jirani na msafiri, kwa wote ni rehema tena ni ujumbe wa amani na mwendeleo mwema. Mafundisho ya Islamu hayaachi taifa lolote katika wanadamu kwa kuwapa mafunzo, bali ni daftari ya mwongozo kwa wale waliopita na watakaokuja baadaye. Jinsi macho ya Mwenyezi Mungu Mjuzi wa ghaibu yanavyotazama chembe zinazokuwa chini ya mawe, na yanafika juu ya nyota zing`aazo mbinguni pia, hivyo mafundisho ya Waislamu yanamaliza haja za wanadamu wanao kuwa masikini na wanyonge na pia inamaliza haja za matajiri na wenye nguvu.

Kwa neno zima, dini ya Kiislam siyo nakala ya dini zilizotangulia. Bali ni kiungo cha mwisho cha mnyororo wa dini, na ni jua la taratibu ya mwenendo wa kiroho. Kweli, kwa jina la dini, dini zote zinashirikiana jinsi alimasi na makaa vinavyo shirikiana jina la *carbon*. Lakini almasi ni almasi na makaa ni makaa, tofauti kubwa. Hivyo kukisia jambo lolote la Islam juu ya jambo lolote la dini zingine ni kosa, si sawa. Jina la jiwe, linatumiwa kwa changarawe na pia linatumiwa kwa marmari. Lakini changarawe ni changarawe na marmari ni marmari. Basi kufikiria kuwa katika dini ya Kiislam inapatikana *Kalimah* hivyo dini zingine pia zitakuwa na *kalimah* ni matokeo ya kutojua na kutoifikiria Qur`an.

Dhuluma kubwa ni hii, baadhi ya watu wamekwisha dai ya kuwa:

*La ilaha illallahu Ibrahimu khalilullah, La ilaha illallahu Musa kalimullah, La ilaha illallahu Isa rahullah ni kalimah* za dini zilizotangulia, hali katika Taurati na Injili na katika vitabu vya Wakristo hazipatikani hata alama ndogo za *kalimah* hizi. Makosa mengi yameingia siku hizi katika Waislamu, lakini je, wamesahau *kalimah* zao? Basi inawezekanaje kusema ya kuwa Wakristo na Wayahudi wamesahau *kalimah* zao, na hata katika vitabu vyao *kalimah* zao zimetoweka, basi ni nani aliyewambia Waislamu *kalimah* hizi? Haki ni hii ya kuwa isipokuwa Mtume Muhammad s.a.w. Hakuna nabii yeyote aliyekuwa na *kalimah*.

Katika sifa za Mtume Muhammada s.a.w. sifa mojawapo ni hii ya kuwa yeye ni nabii wa pekee katika manabii wote aliyepewa *kalimah*. Manabii wengine hawakupata *kalimah*. Kwa maana katika *kalimah* kukiri utume kumeunganishwa na kukiri umoja wa Mungu. Na kukiri umoja wa Mungu ndiyo umoja wa milele usiyoweza kufutika. Zama za manabii waliotangulia zilikadiriwa kumalizika kwenye muda maalum, hivyo Mwenyezi Mungu hakuliunganisha jina lake litajwe pamoja na majina yao. Lakini utume wa Mtume Muhammad s.a.w. ulikadiriwa kuendelea mpaka Kiyama na wakati wake haukuandikwa kwisha; kwa sababu hii Mwenyezi Mungu ameunganisha utume wake na jina lake pamoja na jina lake pamoja na *kalimah* ya Tauhidi ili dunia ipate habari kuwa kama ilivyo *Laa ilaaha illallahu* isiyoweza kufutika, kadhalika *Muhammadur-Rasulullah* haitafutika kamwe.

Ni ajabu, Myahudi hasemi kuwa Musa a.s. alikuwa na *kalimah*, Mkristo hasemi Isa a.s. alikuwa na *kalima*, mfuasi wa Ibrahim a.s. hasemi kuwa Ibrahim alikuwa na *kalimah*. Lakini Mwislamu ambaye nabii wake ametukuka kwa kupewa *kalimah*, na aliyeheshimiwa na Mwenyezi Mungu kwa kumpa *kalimah*, na aliyetukuzwa kuliko mataifa mengine kwa njia ya *kalimah*, Mwislamu huyu kwa ukarimu wa moyo wake anakuwa tayari kuigawanya heshima ya nabii wake katika manabii wengine. Na ambapo wafuasi wa manabii hawa hawadai *kalimah* yoyote, lakini Mwislamu huyu kwa ajili yao anatunga kalima na anaweka mbele ya watu, na anasema hii ilikuwa ya Mayahudi, hii ilikuwa ya Masabii na hii ilikuwa ya Wakristo.

Kwa neno zima, siyo lazima kwa kila dini iwe na *kalimah*. Ingekuwa lazima hata hivyo isingewezekana Waahmadiyya kuwa na *kalimah*, maana Uahmadiyya siyo dini mpya. Uahamadiyya unaamini *kalimah*

ile ile aliyoiweka Mtume Muhammad s.a.w.mbele ya dunia ambayo ni  
*Lailaha illallahu Muhammadur-Rasulullah.*

## **IMANI YA WAAHMADIYYA JUU YA MUNGU NA MTUME WAKE.**

Mbele ya Waahmadiyya Mwumba wa ulimwengu huu ni Mungu Mmoja ambaye ni *Wahdahu la sharika lahu* - hana mshirika. Nguvu na uwezo Wake hauna mipaka. Ndiye Bwana, Mwingi wa rehema na Mwingi wa huruma, Mmiliki wa siku ya malipo. Sifa zote zilizotajwa katika Qur`an zinamhusu Yeye. Yeye ameepekana na mambo yote ambayo Qur`an imemwepusha nayo. Waahmadiyya wanakiri ya kuwa Muhammd s.a.w. bin Abdullah bin Abdul Muttalib, Mkureishi , mwenyeji wa Makka alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, na sheria ya mwisho ikashuka kwake. Yeye akatumwa kwa Waajemi , Waarabu, weupe, weusi, kwa watu wote na kwa mataifa yote, Zama ya utume wake imeenea toka kudai kwake utume mpaka asiwepo juu ya ardhi hata mtu mmoja aliye hai. Mafundisho yake yamelazimishwa kwa kila mwanadamu kuyafuata, na hakuna mtu yeyote aliyekwisha sikia mafundisho yake na hakumkubali na asiwe mwenye kustahili kupata adhabu ya Mungu. Kila mtu ambaye limefika kwake jina lake na zikaelezwa mbele yake dalili za ukweli wake, ni lazima kwake kumwamini, na bila ya kumwamini yeye hana haki ya kupata uokovu. Utakatifu wa kwelikweli haupatikani isipokuwa kwa kumfuata na kushika hatua zake sawasawa.

## **IMANI YA WAAHMADIYYA JUU YA KHATAMUNNUBUWWAT**

Katika hawa wasiojua wako wanaofikiri ya kuwa Waahmadiyya hawakiri Khatamunnuwwat wala hawakubali ya kuwa Mtume Muhammad s.a.w. alikuwa *khatamannubiyyin*, lakini fikara zao za



namna hii zote ni kwa sababu ya kutofahamu. Waahmadiyya wanapojiita Waislamu na wanakiri kwa yakini shahada basi inawezekanaje kusema ya kwamba wao hawakubali *khatamannubuwat* Na wasimwamini Mtume s.a.w. kuwa *Khatamunnabiyyin*? Mwenyezi Mungu amesema waziwazi katia Qur`an Takatifu: *Maa kaana Muhammadaun abaa ahadin min rijaalikum walakin rasuulallaah wa khaatamannabiyyiin*, yaani, Muhammad s.a.w. si baba wa yeyote katika wanaume wenu bali yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na *Khaatamannabiyyin*. Anayeamini Qura`an Takatifu anawezeje kukataa aya hii, basi hii si imani ya Waahmadiyyakabisa ya kuwa Mtume Muhammad s.a.w. *naudhu bilah* (Mungu apishe mbali), hakuwa *Khatammnabiyyiin*. Waahmadiyya hawasemi ila hivi ya kuwa maana ya *khatamannabiyyiin* inayojulikana siku hizi kati ya Waislamu haipatani na aya hii iliyotajwa juu wala haionekani heshima ya Muhammad s.a.w. katika maana hiyo namna ilivyokadiriwa katika aya hii heshima ya Mtume s.a.w. Kwahiyo, jamaa Ahmadiyya wanaifasiri aya hii kwa tafsiri inayojulikana sana katika lugha ya Kiarabu, na pia tafsiri hii inahakikishwa kwa maneno ya Seyidatina Aisha, Seyyidna Ali, na kwa maneno ya masahaba wengine. Ndiyo tafsiri ambayo kwa kuikubali bila shaka shani na heshima ya Mtume Muhammad s.a.w. inazidi sana, na unahakikishwa utukufu wake zaidi kuliko wanadamu wote wa ulimwengu. Basi Waahmadiyya hawaikatai *khatamunnubuwat* bali wanaikataa maana inayoingizwa na Waislamu kwa kosa, waila kukataa *Khatamannubuwat* ni kufuru. Na Waahmadiyya kwa fadhili za Mwenyezi Mungu ni Waislamu, na kwa kushika Islam wanaifahamu ndiyo njia moja tu ya kupata uwokovu.

Katika hawa watu wasiojua, pengine wako wanaodhani ya kuwa Waahmadiyya hawaiamini sawasawa Qur`an Takatifu, bali wanazikubali juzu chache tu. Juzi nilipokuwa katika mji wa Queta (Pakistan) watu wengi waliokuja kuonana nami wakaniambia ya kwamba wao wameambiwa na Masheikh wao ya kuwa Waahmadiyya hawaiamini Qur`an nzima. Haya pia ni masingizio ambayo maadui wa Ahmadiyya wanawasingizia Waahmadiyya . Hali Wahmadiyya wanaiamini Qur`an na waifahamu ndicho kitabu kisichoweza kubadilishwa wala kutanguliwa kabisa. Ahmadiyya wanafahamu kila neno toka *be ya bismillahi* mpaka *sin* ya *wannasi* limetoka kwa .Mwenyezi Mungu na linatakiwa kufuatwa.

## IMANI YA WAAHMADIYYA JUU YA MALAIKA.

Katika hawa watu wasiofahamu Ahmadiyya wako baadhi yao wanaowasingizia Waahmadiyya ya kuwa hawaamini Malaika wala hawakiri ya kuwa yuko shetani. Masingizio haya pia ni ya uwongo, maana habari za Malaika ziko katika Qur`an Takatafu na habari za shetani pia humo zimetajwa. Basi mambo yaliyotajwa katika Qur`an kwa kuiamini Qura`an inawezekanaje Waahmadiyya kuyakataa? Sisi kwa rehema za Mwenyezi Mungu tunaamini sawasawa ya kuwa wako Malaika, bali tunaweza kusema baraka tulizopata kwa kuifuata Ahmadiyya zimekuwa sababu ya kuwaamini Malaika, siyo haya tu bali tunakubali kwa yakini kuwa tunaweza kupata urafiki wa Malaika kwa msaada wa Qur`an, na inawezekana kufunzwa nao elimu ya kiungu.

Mimi mwandikaji wa maneno haya nimefunzwa na Malaika elimu za namna nyingi. Safari moja, Malaika mmoja akanifundisha maelezo ya sura ya *Alhamdu*. Tangu wakati ule mpaka sasa maelezo na tafsiri ya sura hii imefunuliwa kwangu kwa hesabu isiyo kiasi. Mimi kwa rehema za Mungu nadai ya kwamba naweza kutoa maelezo kamili ya maana mbalimbali juu ya habari yoyote ya kiungu katika sura hii fupi ya *Alhamdu* kwa namna ambayo mtu wa dini yoyote na madhehebu yoyote hawezi kutoa maelezo kama hayo katika kitabu kizima cha dini yake. Tangu muda mrefu nimetangaza madai haya lakini hata mtu mmoja hajapata kupokea mashindano ya jambo hili. Dalili za kuhakikisha ya kuwa Mwenyezi Mungu yupo; dalili za Umoja wa Mwenyezi Mungu; dalili za utume na haja yake; hakika ya dua na kudra ya Mwenyezi Mungu kufufuka na mkusanyiko wa Akhera, Pepo na Jahannam; habari hizi zote zinaweza kuhakikishwa katika sura ya *Alhamdu* kwa namna ambayo hata kurasa mamia na mamia za vitabu vingine haziwezi kutoa mfano wake. Basi si swali la kuwakataa Malaika, bali Waahmadiyya wanadai ya kuwa wanapata faida kwa Malaika.

Ama shauri la shetani, basi jueni shetani ni kitu kichafu. Kuamini shetani haina maana. Naam, katika Qur`an inajulikana ya kwamba yuko shetani. Siyo haya tu bali pia tunafahamu ya kwamba Mwenyezi Mungu ametulazimisha tuvunje nguvu za shetani na tufute utawala wake. Mimi pia nimemwona shetani katika ru`ya hata nikashikana naye mieleka, na kwa msaada wa Mwenyezi Mungu na baraka za kalimah ya *taawudh* (kusema): *Audhu billah minashaitanir-rajim* nikamshinda. Na pia

safari moja Mwenyezi Mungu akaniambia ya kuwa kazi uliyolazimishwa kuifanya shetani na wafuasi wake wataikingikia vizuwizi vingi ili isiendelee. Lakini wewe usiwajali na endelea mbele kwa kusema: "Kwa fadhili na rehema za Mwenyezi Mungu." Hapo nikaendelea kufika mahali ambapo Mwenyezi Mungu aliniambia kufika. Basi nikamkuta shetani na wafuasi wake. Wakaanza kuniogopesha na kunitisha kwa namna mbalimbali. Pahali fulani wao walikuja mbele yangu na walifanya bidii kuniogopesha. Pahali fulani walikuwa wanakuja mwili mtupu. Pengine mashetani walikuwa wanakuja kwa sura ya simba au chui au tembo. Lakini kwa kushika amri ya Mungu mimi sikuwajali, na kwa kusema, "Kwa fadhili na rehema za Mwenyezi Mungu" nikaendelea mbele na mbele. Nilipokuwa nayasema maneno haya, shetani na wafuasi wake walikuwa wanakimbia na kiwanja kikabaki cheupe. Lakini tena baada ya muda mfupi kwa sura mpya na hali nyingine alikuwa anakuja mbele yangu, na kwa kuishika hali hii ya kusema maneno ya juu nilikuwa nashinda. Mwisho nikafika pahali palipokusudiwa. Na shetani akaacha kiwanja na akakimbia kabisa. Basi kwa kufuata njozi hii mimi naandika juu ya kila makala yangu yenye maana, "Kwa fadhili na rehema za Mwenyezi Mungu." Basi sisi tunawaamini Malaika na tunakiri ya kuwa Shetani yupo.

Baadhi ya watu wanasema ya kuwa Waahmadiyya hawakubali miujiza. Hii pia ni kinyume cha haki. Licha ya miujiza ya Mtume Muhmmad s.a.w. sisi pia tunakubali ya kuwa wafuasi wa Mtume Muhammad s.a.w. vilevile wanaweza kupata miujiza. Qur`an nzima imejaa miujiza ya Mtume wetu Muhammad s.a.w.; na mtu yeyote hawezi kuikataa isipokuwa kipofu wa milele.

## **IMANI YA WAAHMADIYYA JUU YA UWOKOVU**

Baadhi ya watu wanakosa kufahamu ya kuwa tunaamini ati watu wote ni wa motoni isipokuwa Waahmadiyya tu. Lakini kufahamu namna hii pia ni matokeo ya ujinga au uwadui walio nao mioyoni mwao juu ya Waahmadiyya. Mbele yetu hata inawezekana mtu mmoja awe Ahmadiyya lakini aingie jahanam, kama inavyowezekana mtu mmoja asiwe Ahmadiyya na aingie peponi. Maana, pepo haipatikani kwa kukiri kwa ulimi tu, bali pepo inapatikana, baada ya kumaliza wajibu mwingi,

hivyo kukataa kwa ulimi hakumtupi mtu motoni bali kwa kutupwa motoni yako mambo mengi. Mtu yeyote hawezi kutupwa motoni mpaka afundishwe sawasawa, haidhuru hata awe mkataaji wa ukweli ulio mkuu. Mtume Muhammad s.a.w. anasema: Anayekufa katika utoto wake au watu wanaokaa juu ya mlima mrefu au wakao katika pori au wazee wasio na akili zaidi au wehu, wao hataulizwa maana hawakujua habari zaidi. Bali Mwenyezi Mungu atamtuma nabii siku ya Kiyama kwa ajili ya watu wa namna hii na wao watapewa nafasi kwa kutambua haki na uwongo. Basi hapo baada ya kufahamishwa wataingia motoni na atakayeshika mwongozo atakwenda peponi. Hivyo kusema ya kuwa Waahmadiyya wanaamini ya kuwa kila mtu asiyeingia katika Ahmadiyya ni mtu wa motoni ni uwongo kabisa.

Sisi tuna itikadi ya uwokovu ya kuwa kila mtu anayejizuia kufahamu ukweli na anafanya juhudi ili ukweli usiingie katika masikio yake na asishike mwongozo, au mtu aliyefahamishwa sawasawa na asiamini, mbele ya Mweyezi Mungu mtu ni mkosefu na ataulizwa. Ni dhahiri Mwenyezi Mungu pia ana hayari kumsamehe mtu huyu. Mgawanyo wa rehema zake hauko mikononi mwetu. Mtumishi ni mtumwa, ana haki gani kumzuia bwana wake apendapo kufanya ukarimu? Mwenyezi Mungu ndiye Bwana wetu na Mfalme wetu, naye ndiye Mwumba wetu na Mmiliki wetu. Kama hekima Yake na elimu na rehema Yake ikipenda kumsamehe mtu ambaye kwa hali yake ya siku zote inaonekana haiwezekani kupewa msamaha, basi sisi ni nani tumzuie mkono Wake na tuna haki gani kumkataza asitoe samahani?

Imani ya Waahmadiyya juu ya uwokovu ina wasaa, hata kwa kutazama wasaa wake baadhi ya Masheikh na Waalimu wakaanza kuwaita Waahmadiyya makafiri, maana sisi tunakiri mtu yeyote hataingia katika jahanamu kukaa humo kabisa asitoke tena akiwa anayeamini au kafiri. Sababu Mwenyezi Mungu amesema katika Quran Tukufu: *Rahmatii wasi`at kulla shay-in* "Rehema Yangu imekizunguka kila kitu." Tena amesema: *Ummuhuu haawiyah*, yaani yatakuwa maungano kati ya kafiri na jahannamu kama yalivyo maungano kati ya mama na mtoto wake. Tena amesema: *Maa khalaqtul jinna wal insa illaa liya`buduuni*, "Nimewaumba wote Jinn na Insi ili wawe watumishi wangu." Kwa kuzitazama aya hizi na zingine za namna hii tunawezaje kusema ya kuwa rehema za Mwenyezi Mungu hazitawaafunika wakosefu, na aliyomo katika jahannamu hatatoka? Na watu ambao

Mwenyezi Mungu amewaumba kuwafanya watumishi Wake wawe watumishi wa shetani milele wala wasiwe watumishi wa Mwenyezi Mungu? Na inawezaje kukubaliwa ya kuwa sauti yenye mapenzi ya Mwenyezi Mungu haitawaita: *Fadhulii fii `ibaadii wadkulii jannatii* "Njoooni, ingieni katika watumishi Wangu na ingieni katika pepo Yangu"?

## **IMANI YA WAAHMADIYYA JUU YA HADITHI ZA MTUME S.A.W.**

Baadhi ya watu wanadhani ya kwamba Wahmadiyya hawazikubali hadithi za Mtume s.a.w. Wengine wanawasingizia ya kuwa hawaamini Maimamu wa Fik-ha. Mambo haya yote mawili si haki. Kwa hakika Waahmadiyya wanashika mwendo wa katikati. Hawashiki kama kipofu wala hawakatai kwa ushupavu. Mafundisho kama ya Kiahmadiyya ni haya ya kuwa jambo lililothibitika kwa maneno ya Mtume Muhammad s.a.w. lishikwe na kuyashika maneno ya watu wengine baada ya kusikia maneno ya Mtume s.a.w. haina maana nyingine isipokuwa kuvunja heshima ya Mtume s.a.w. Haiwezekani kusikiliza maneno ya mtumishi mbele ya bwana. Haiwezekani kujifunza kwa mwanafunzi hali Mwalimu mwenyewe yupo. Maimamu wa Fik-ha haidhuru wawe na heshima ya namna gani, lakini bila shaka wao ni wanafunzi na watumishi wa Mtume s.a.w. Na heshima yao yote ilikuwa kwa kumfuata mtume s.a.w. na utukufu wao ulikuwa kwa kumtumikia Mtume s.a.w. Basi jambo lolote linapothibitika kwa Mtume s.a.w. na alama ya kuonesha kuwa jambo hili limesemwa na Mtume s.a.w. ni hii ya kuwa jamo hilo lipatane na kauli ya Mwenyezi Mungu; basi jambo la namna hii linakuwa hukumu ya mwisho na amri isiyoweza kuvunjwa na hakuna mtu mwenye haki ya kuikataa au aseme kinyume chake. Lakini wasimuliao hadithi ni wanadamu, miongoni mwao wako watu wema na wengine waovu, wengine wenye ubongo mzuri na wengine wasio na ubongo mzuri. Wako wenye akili hasa, na wengine wasio na akili zaidi. Katika hali ya namna hii hadithi yoyote inayokuwa kinyume cha Qur`an Tukufu na hali Qur`an ni kitabu kisicho na shaka hata kidogo katika materemsho yake kutoka kwa Mungu, hadithi ya namna hii haitakubaliwa. Lakini hadithi, kama Maimamu wenyewe wanavyokubali, zingine ni za shaka, zingine

zimetungwa na watu wenyewe, kwahiyo mbele ya Qur`an Tukufu bila shaka hadithi za namna hii hazitakubaliwa.

Na kama yasipatikane maneno wazi juu ya jambo fulani katika Qur`ani, na hadithi pia ziwe kwa hali ya dhana, lakini ziwe na maana nyingi, basi hapo Maimamu wana haki gani watoe rai yao na rai yao itakubaliwa. Maana wao wamemaliza maisha yao kwa kufikiri Qur`an na kufikiri Hadithi za Mtume s.a.w. Na rai ya mtu mwingine haitasikilizwa mbele ya rai ya Maimamu. Maana yeye hajawahi kufikiri Qur`an wala Hadithi wala hana elimu na akili ambayo imsaidie kwa kutoa rai na kufikiri sawasawa. Na kama mtu wa namna hii atasema Imamu Abu Hanifa, au Imamu Ahmad au Imamu Shafi au Imamu Malik au Maimamu wengine wana haki gani ya kuwa shauri lao au rai yao ifuatwe, wao ni Waislamu na mimi pia ni Mwislamu. Lakini kama daktari na mtu mwingine wanaanza kuhitilafiana katika maradhi fulani bila shaka shauri la daktari litakubaliwa kuliko shauri la mtu mwingine katika maradhi yale. Kama hitilafu itokee katika jambo la kanuni basi hukumu ya wakili itakubaliwa kuliko hukumu ya mtu asiye wakili. Basi kwa sababu gani tena isishikwe rai ya Maimamu katika mambo ya dini ambao wamemaliza maisha yao kwa kufikiri Qur`an na Hadithi na pia nguvu za ubongo na akili zao ni bora kuliko watu malaki na malaki, bali pia utawa na utakatifu wao umehakikishwa kwa alama iliyotoka kwa Mwenyezi Mungu?

Kwa neno zima Ahmadiyya haisaidii wale wanaoshika Hadithi kwa namna ambayo hata wanavunja aya za Qur`an na heshima yake, wala haiwasaidii wale wanaoziacha hadithi kabisa; bali Waahmadiyya wanashika njia iliyo sawa na rahisi na iliyoshikwa na Imamu Abu Hanifa ya kuwa Qur`an ni mbele kuliko vyote. Baada ya Qur`an Hadithi zilizo sahihi na baada ya haya katika daraja ya tatu rai ya Imamu, yaani fundi mkubwa wa elimu ya dini. Kwa sababu hii Waahmadiyya pengine wanajiita *Hanafi*, siyo maana yake isipokuwa tunakubali jinsi Imamu Abu Hanifa alivyoeleza asili ya dini. Pengine Waahmadiyya wanajiita *Ahli Hadith*, sababu mbele ya Waahmadiyya kauli ya Mtume Muhammad s.a.w. kama ithibitike inakuwa bora kuliko ya wanadamu wote wa ulimwengu, hata kuliko kauli za Maimamu.

## **IMANI YA WAAHMADIYYA JUU YA KUDRA YA MWENYEZI MUNGU**

Katika makosa yaliyoenea sana katika watu wasiojua Ahmadiyya, mojawapo ni hili ya kwamba Waahmadiyya wanaikataa kudra ya Mwenyezi Mungu. Ama kwa hakika Wahmadiyya si wenye kukataa kudra ya Mwenyezi Mungu kwamwe. Tunaamini ya kuwa kudra ya Mwenyezi Mungu inaendelea katika dunia hii na itaendelea mpaka siku ya Kiyama, na hapana anayeweza kubadilisha kipimo chake. Sisi tunakataa jambo hili tu ya kuwa wivi wa wevi, asiyesali kuacha kwake sala, uwongo wa mwongo, udanganyifu wa adanganyaye, uaji wa auaye, na ouvu wa mwovu uelekezwe kwa Mwenyezi Mungu. Mbele yetu Mwenyezi Mungu ameendesha pamoja katika wakati mmoja mifereji miwili - wa *Takdir* (kudra) na *Tadbir* (hila), Na ameweka katikati yo kizuio isiunganike pamoja. Kiwanja cha *Tadbir* ni pahali pake, na kiwanja cha *Takdir* ni pajhali pake. Mambo aliyoyapitisha Mwenyezi Mungu kwa kudra yeke, basi hila haiwezi kufanya chochote. Mambo aliyoyapitisha kufanywa kwa hila, katika mambo ya namna hii mtu kwa kuitegemea *takdir* anaharibu akhera yake. Basi sisi tunayoyakataa ni haya ya kuwa mwanadamu anafanya bidii kuvificha vitendo vyake vibaya nyuma ya pazia ya takdir. Na uovu na upotevu wake anaufanya kuwa halali kwa sababu ya neno la *takdir*. Na pahali ambapo Mwenyezi Mungu ametoa amri ya kufanya hila yeye anaitegemea *takdir*. Kwa sababu matokeo ya mwendo wa namna hii kila mara yanakuwa ya hatari. Waislamu waliendelea kuitegema *takdir* na wakaacha kufanya juhudi iliyo ni lazima kwa ustawi wa taifa, na hivyo walioacha dini wakapata hasara duniani pia. Wangeangalia kuishika hila na juhudi katika mambo ambayo Mwenyezi Mungu amewahimiza, kwa bidii, wasingenguka wala wasingepata hali mbaya namna hii kama sasa.

## **IMANI YA WAAHMADIYYA JUU YA JIHADI**

Kosa jingine lililoenea ni shauri la jihadi. Wako watu wanaosema ya kwamba Waahmadiyya wanaikataa jihadi. Lakini sivyo. Waahmadiyya hawaikatai jihadi. Waahmadiyya. Wanayoyasema ni haya; vita vinakuwa namna mbili. Vita moja ni ya jihadi, na vita nyingine ni vita tu. Vita ya

jihadi ni vita inayopiganwa kwa sababu ya kulinda dini, na kushindana na maadui wanaotaka kufuta au kuingamiza dini kwa upanga, na wanataka kuibadilisha imani ya watu kwa ncha ya jambia. Kama matukio ya namna hii yatukie katika dunia, basi vita vya jihadi vinakuwa lazima juu ya kila Mwislamu. Lakini ina sharti moja ya kuwa tangazo la jihadi ya namna hii litangazwe na Imamu (mkubwa na kiongozi wa jamia) ili Waislamu wajue nani anatakiwa kuingia katika jihadi hii na nani wanatakiwa kungoja zamu yao. Kama haitakuwa namna hii, basi kila Mwislamu asiyeingia katika jihad atakuwa na dhambi. Lakini kama itatangazwa na Imamu, Mwislamu atakayekuwa na dhambi ni yule ambaye anaitwa lakini hahudhurii katika jihad. Waahmadiyya walipokuwa wanaikataa vita ya jihadi walikuwa wakikataa kwa sababu Waingereza hawakuwa wenye bidii ya kubadilisha dini za watu kwa nguvu ya upanga. Lakini kama mawazo haya ya Waahmadiyya yalikuwa kosa, na Waingereza walikuwa wanatumia nguvu ya upanga kwa kubadilisha dini za watu, kwa nini hawa Waislamu walikaa kimya hawakushika upanga na kushindana nao ilipokuwa kwa fikira zao ilionekana kuwa jihadi imelazimika? Kama hawakuingia katika jihadi, Wahmadiyya watasema mbele ya Mwenyezi Mungu ya kuwa hawakuingia kwa sababu hayakuwako mambo ya kulazimisha jihadi. Lakini hawa Waislamu watajibu nini mbele ya Mwenyezi Mungu hali walikuwa wanajua jihadi imelazimika nao hawakuingia? Je, watasema: Ee Mola wetu tunajua kwa yakini wakati huu hasa ni wa jihadi, na tulikuwa tukifahamu jihadi imekwisha lazimika, lakini Ee Mola wetu sisi hatukufanya jihadi sababu mioyo yetu ilikuwa inaona hofu wala hatukuwaambia wale wasiokua na hofu kwenda katika jihadi, sababu tulikuwa tunaogopa kama tutawaambia wengine, Waingereza watatukamata na kutufunga. Sitaki kukata hukumu mimi, bali nawaachia watu wenye akili kukata hukumu juu ya jambo hili. Jibu gani, letu au lao, litakalokuwa na haki ya kukubaliwa mbele za Mwenyezi Mungu?

Mpaka sasa nimesema kwa ajili ya wale wasiojua zaidi habari za Ahmadiyya na wanasikia kwa maadui, na bila kufikiri wanataka kutunga maneno kadhaa wa kadhaa na kusema hii ndiyo imani na mafundisho ya Waahmadiyya. Baada ya kutoa majibu ya wasiwasi wa hawa watu nataka kuzungumza na wale waliosoma habari za Ahmadiyya na wanafahamu ya kuwa Waahmadiyya wanaamini umoja wa Mwenyezi Mungu na wanaamini utume wa Mtume Muhammad s.a.w. na



wanaamini Qur`an pia, wanakubali Hadithi za Mtume s.a.w., wanasali na kufunga saumu, wanakwenda Makka kuhiji na wanatoa Zaka. Wanaamini habari za Kiyama - kufufuka, thawabu na adhabu. Lakini wanashangaa kama Waahmadiyya ni Waislamu safi sawa na Waislamu wengine, kwa nini firka mpya imeanzishwa? Mbele ya hawa watu, imani ya Waahmadiyya na vitendo vyao hayana lawama lakini kuanzisha firka mpya ndilo jambo la lawama, maana kama hakuna tofauti, basi imekuwa sababu gani ya kuleta hitilafu tena? Na kama hitilafu hakuna, basi tena imekuwako kusudi gani ya kutengeneza msikiti mwingine?

### **SABABU YA KUENZISHA FIRKA NYINGINE.**

Swali hili linawezekana kujibiwa kwa namna mbili. Kwanza kwa ya akili na kwa njia ya kidini. kwa njia ya akili, jawabu lake ni hili ya kuwa firka au Jamia siyo jina la idadi. Watu wawe elfu, laki, hata laki mia, hawaitwi Jamia. Bali Jamia ni jina la watu ambao kwa umoja wao wamekwisha kata hukumu ya kuwa watafanya kazi pamoja, na kwa Mwendeleo na taratibu maalumu wamekwisha anzisha kazi yao. Watu wa namna hii hata wawe watano au saba watakuwa Jamia. Na watu wasiokuwa na jambo hili haidhuru hata wawe milioni na milioni hawataitwa jamia. Mtume Muhammad s.a.w. alipodai katika Makka, siku ya kwanza waliomwamini walikuwa watu wanne tu na yeye mwenyewe alikuwa wa tano. Ingawa walikuwa watano tu, wao walikuwa jamia, lakini makafiri wa Makka walikuwa karibu elfu kumi hawakuwa na Jamia. waala Waarabu wote hawakuwa jamia, sababu hawakuwa katika umoja wala hawakukata hukumu ya kufanya kazi kwa umoja, wala hawakuwa na mwendeleo maalumu. Wala Waarabu hawakukata hukumu ya kufanya kazi kwa umoja na ikawa taratibu moja, wala hawakuwa na mwendeleo maalum. Basi kabla ya kuuliza swali la namna hii inatakiwa kufikiriwa: je, katika wakati huu Waislamu wako katika hali ya *Jamia*? Je, Waislamu wa dunia nzima wamekwisha kata hukumu ya kuwa watafanya kazi katika mambo yote ya ulimwengu kwa umoja? Au je, wanao mwendeleo na taratibu maalum ya kazi? Kwa kuhurumiana tu nakubali ya kuwa kweli Waislamu wanahurumiana. Lakini huruma hi pia haipatikani katika Waislam wote. Wengine hawana huruma na wengine baadhi yao wanahurumiana sana. Na pia hakuna

taratibu maalum ambayo kwa kuishika hitilafu zilizoko baina ya Waislamu zifutike. Naam, nakubali ya kuwa hitilafu siku zingine inatokea katika jamia pia. Hata katika jamia za wakati wa manabii hitilafu hupatikana. Katika siku za Mtume Muhammad s.a.w. safari moja ikatokea hitilafu kati ya Ansar na Muhajirin. Na pengine ikatokea hitilafu katika makabila fulani fulani. Lakini Mtume Muhammad s.a.w. alipotoa hukumu ndipo hitilafu zote zilikwisha. Hivyo katika siku za Makhalifa baadhi ya wakati hitilafu zilikuwa zinatokea, lakini walipokata hukumu hitilafu zilikwisha. Karibu miaka 70 baada ya siku za Makhalifa Waislamu walikaa chini ya ufalme mmoja, na kila pahali Waislamu walipokuwa wanakaa walikuwa katika mwendeleo na taratibu maalum. Mwendeleo huo ingawa ulikuwa m`baya au mzuri, lakini uliwaweka Waislamu katika hali ya umoja. Baadaye ilitokea hitilafu na Waislamu wakagawanyika katika sehemu mbili. Waislamu walikuwa wanakaa katika nchi ya Spain wakawa sehemu moja, na Waislamu wa pande zingine wakawa sehemu ya pili. Ingawa hitilafu hii haikuwa kubwa, juu ya hayo sehemu kubwa ya Waislamu walikuwa wanaendelea kwa ummoja chini ya taratibu maalum. Lakini ilipopita miaka mia tatu taratibu hii ikavunjika-vunjika hata Waislamu wote wamegawanyika-gawanyika. Ukatokea mfarakano mkubwa.

Mtume s.a.w. alisema haki: *Khairul kuruni karni, thummalladhina yalunahum, thummalladhina yalunaham, thumma yafshul kidhbu,*" yaani karne bora ni karne yangu, kisha watakaokuwa watu wazuri ni wale wawafuatao wa karne ya pili, tena wale wawafuatao wa karne ya tatu, kisha ukweli utafutika, uongo na dhuluma na jeuri na hitilafu zitatokea. Na yote haya yakatokea kama yalivyosemwa. Na hitilafu ikaendelea hata katika miaka mia tatu hii iliyopita. Waislamu wamekwisha poteza nguvu yao kabisa. Nakumbuka siku ambazo Ulaya nzima ilikuwa inamwogopa mfalme mmoja mmoja wa Waislamu, lakini sasa Waislamu wa ulimwengu wote hawana nguvu ya kushindana hata na ufalme mmoja wa Ulaya na Amerika. Utawala wa Kiyahudi uliosimamishwa juu juu katika nchi ya Palestina, ijapokuwa ni mdogo sana, lakini majeshi ya Sham, Iraq, Lebanon, Saudi Arabia, Misri na Palestina yanashindana na kupigana nao, juu ya hayo Mayahudi wamekamata sehemu zaidi ya nchi ya Palestina kuliko waliyopewa na Umoja wa Mataifa (U.N.O.). Ni kweli ya kwamba ufalme wa Kiyahudi unasaidiwa na Amerika na Uingereza. Ndilo hilo tulilosema ya kuwa

siku moja ufalme mmoja wa Kiislam ulikuwa unashinda juu ya Ulaya nzima, lakini sasa baadhi ya serikali za Ulaya zina nguvu zaidi kuliko Waislamu wote.

Basi hakuna sasa jamia katika Waislamu sawa na maana ya jamia kama ilivyoielezwa juu. Naam, ziko serikali za Kiislam na serikali kubwa kuliko serikali zingine za Kiislam ni serikali ya Pakistan, iliyosimamishwa juzujuzi kwa fadhila za Mwenyezi Mungu. Lakini Islamu si jina la Pakistan, wala si jina la Misri, wala Islam si jina la Ajemi, wala Islam si jina la Afghanistan, wala si jina la Saudi Arabia; bali Islam ni jina la taratibu ya umoja iliyowakusanya Waislam wote katika umoja. Na taratibu ya namna hii haipatikani sasa katika dunia. Pakistan ina huruma na Afghanistan, Afghanistan pia ina huruma na Pakistan. Lakini Pakistani haiko tayari kukubali kila jambo la Afghanistan, wala Afghanistan haiko tayari kukubali kila jambo la Pakistan. Sasa serikali zote mbili ni mbalimbali, na wako huru katika mambo yanayohusu nchi zao; hii ndiyo haki ya watu. Watu wa Afghanistan ni waungwana pahali pao na wenyeji wa Pakistan wana uhuru pahali pao. Watu wa Misri pia ni waungwana mahali pao, hakuna taratibu inayoweza kuwaweka katika kamba moja.

Basi katika wakati huu wako Waislamu na pia ziko serikali za Kiislam. Na serikali zingine za Kiislam kwa rehema za Mungu zinaendelea vizuri. Lakini juu ya hayo Waislamu si Jamia moja. Mathalan manowari za Pakistan ziwe madhubuti sana hata bahari yote ya Hindi iwe chini ya ulinzi wake. Na majeshi yake yawe na nguvu hata itetemeke serikali ya India. Uwezo wa mali yake uendelee mbele hata ukamate soko za duniani, bali uendelee mbele hata kuishinda Amerika. Je, serikali ya Ajemi, Sham, Palestine na ya Misri zitakubali kujiunga katika serikali ya Pakistan? Ni dhahiri hawatakubali. Bila shaka serikali hizi zitakuwa tayari kuikubali heshima ya Pakistan. Zitakuwa tayari kuihurumia Pakistan. Lakini hazitakuwa tayari kujiingiza ziwe sehemu ya utawala wa Pakistan. Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu hali ya siasa za Waislamu inaendelea kuwa bora, na serikali zingine mpya za Kiislam zinasimamishwa. Lakini juu ya hayo Waislamu wa ulimwengu wa dunia nzima hawawezi kuitwa jamia, maana wote wamegawanyika katika siasa mbalimbali na wamegawanyika katika serikali mbalimbali. Hakuna taratibu inayoweza kuzikusanya sauti zao pahali pamoja. Hali Islam inadai ya kwamba ni dini ya ulimwengu mzima. Islam si jina la Waislamu wa Bara Arabu. Islam si jina la waislamu wa nchi ya Sham, wala Islam

si jina la Waislamu wa Bara la Ajemi. Islamu si jina la Waislamu wa Afghanistan. Ambapo Waislamu wa kila bara ya dunia wanakusanyika chini ya jina la Islam. Hivyo jamia ya Islam inaweza kuwa ile inayoweza kuwakusanya firka zote, na mpaka isimamishwe jamia ya namna hii hatuna budi kusema ya kuwa Waislamu hawana jamia ingawa uko ufalme na ipo serikali.

Hivyo Waislamu hawana mwendeleo na taratibu maalumu kama walivyo hawana umoja maalumu. Waislamu hawana mpango wa mambo ya siasa wala wa utamaduni wala wa dini. Kushindana na maadui wa Waislamu kila mtu peke yake si kitu. Lakini kushindana kwa taratibu maalumu na kupeleleza hali ya maadui, na kuzivunja hila zao pande zote kwa mwendeleo na taratibu maalumu ni shauri jingine. Basi kwa hali ya Mwendeleo na taratibu Waislamu wa sasa pia hawana jamia.

Kwa kuyashika mambo haya yote mawili yaliyotajwa juu kama Jamia yoyote inaanzishwa haiwezekani kulaumiwa na kusemwa ya kwamba kwa nini jamia mpya imeanzishwa. Bali inatakiwa kusemwa ya kwamba kwanza haikuwako jamia yoyote na sasa imeanzishwa jamia moja. Mimi nawambia hawa marafiki wenye wasiwasi mioyoni mwao ya kuwa Waahmadiyya wanaposhika sala na Kibla na Qur`an na Mtume s.a.w. kwa nini wameanzisha jamia mpya? Wanatakiwa kufikiri juu ya jambo hili kuwa wakati umefika kuifanya Islam jamia moja. Itangojewa mpaka lini kwa kazi hii? Serikali ya Misri imeshughulika katika kazi yake pahali pake. Serikali ya Ajemi inaendelea mahali pake kufanya kazi yake, na Serikali zingine za Kiislam pia zimeshughulika kazi zao mahali pao. Lakini juu ya hayo uko upungufu unaonekana na kwa kuimaliza upungufu huu Jamia Ahmadiyya imeanzishwa .

Waturuki walipovunja taratibu ya Khilafat (Ukhalifu) baadhi ya wanazuoni wa Misri (kwa kuhimizwa na mfalme wa Misri) wakaanzisha taratibu ya Khilafat; na ilikuwa makusudio yao Waislam wa ulimwengu wamtambue mfalme wa Misri kama ni Khalifatul-Muslimin, na hivyo nchi ya Misri itukuke kuliko nchi za Waislamu wengine lakini Saudi Arabia ikaanza kufanyia shauri hili upinzani na kusema ya kuwa shauri hili kwa hakika limeanzishwa kwa kuhimizwa na Waingereza kwa siri. Mtu yeyote kama anastahili kuwa Khalifa basi si mwingine bali ni mfalme wa Saudi Arabia (nchi ambayo ndani yake imo Makka na Madina). Hakuna shaka ya kuwa taratibu ya Khilafat ndiyo silka ya muungano ambayo kwa kuishika Waislamu wote wanaweza kuungana pamoja lakini

neni la Khilafat lilipohusika na mfalme maalumu, wafalme wengine wa Kiislamu wakafahamu mara moja ya kwamba kwa njia hii ipo nia ya kutaka kuingiza machafuko katika serikali zao, na taratibu hii iwe dini tu bila sha ushindi wa kitawala hautatokea. Maana kwa sababu ya ushindani wa kitawala taratibu ile iliyokuwa ya faida ikavunjika isiendeleo, Lakini kama mwendeleo na taratibu ya namna hii isimamishwe katika watu tu wasiyo wafalme na msingi wa taratibu ile itakomea katika nchi ile ile tu ambayo serikali yake inasaidia. Lakini ushindani wa kidini hautafanya mwendeleo huo ukome katika nchi moja tu, bali utafika katika kila nyumba na utaimarisha mizizi yake hata katika nchi zisizo na serikali za Kiislamu. Serikali za nchi hizi hazitaleta uwadui juu ya mwendeleo na taratibu za namna hii, sababu hautakuwapo ushindani wa kitawala.

Historia ya Kiahmadiyya ni shahidi juu ya jambo hili. Uahamadiyya haukuwa na makusudio mengine ila kuwaungani sha Waislamu. Haukutafuta mambo ya kifalme wala haukuwa na nia ya kupata utawala. Waingereza wakati mwingine wakaitia Ahmadiyya katika taabu na mashaka. Lakini kwa kuona msingi wa Ahmadiyya ni dini, si makusudio yao kuingia katika mambo ya utawalaa, hawakuwaletea Waahmadiyya upinzani wa dhahiri. Katika nchi ya Afghanistan, baadhi ya wafalme wakaleta udhia juu ya Waahmadiyya kwa sababu ya hofu ya Masheikh wao. Lakini katika mkutano wao wa siri wakatoa udhuru na wakajuta. Hivyo katika nchi zingine za Kiislamu watu wakaleta upinzani, Masheikh wao pia wakaleta uwadui, na Serikali zao kwa kuwaogopa watu wao pia zikatia mizingili katika mwendeleo wa Ahmadiyya. Lakini juu ya hayo Serikali yoyote haikufahamu ya kwamba Mwendeleo wa Ahmadiyya umesimamishwa kuvunja utawala wao. Na mawazo yao yalikuwa haki kabisa, kwani Ahmadiyya haina mwungano na mambo ya kitawala. Ahmadiyya imeanzishwa kwa kuitengeneza sawasawa hali ya kidini ya Waislamu, na kuwaingiza Waislamu katika silka ya umoja ili kwa kuungana pamoja washindane na maadui wa Uislam kwa silaha za tabia njema na za kiroho.

Kwa kulifahamu jambo hili hili Wabashiri wa Kiahmadiyya wakafika katika nchi ya Amerika watu wa hukowakaleta upinzani juu ya ubashiri wa Kiahmadiyya kadiri ile wanaofanya juu ya watu wa Asia. Lakini walipoangalia na wakaona ni mwendeleo wa kidini hawakuonesha uwadui. Serikali ya Kiholanzi pia ikashika njia hii hii katika nchi ya

Indonesia. Ilipoona Waahmadiyya hawaingii katika mambo ya kitawala, ijapokuwa ilipeleleza kwa siri kutaka kujua Waahmadiyya wanafanya nini, wala haikuwahurumia, lakini pia haikuona haja ya kuleta upinzani wa dhahiri kwa Waahmadiyya. Waholanzi walikuwa na haki katika mwendeleo wao wa namna hii, maana sisi tulikuwa tunaibashiri Islam iliyo ni kinyume cha dini yao. Kwahiyo hatustahili sana kupata huruma yao. Wala sisi hatukuwa wenye kuingia katika mambo yao ya kitawala, kwahiyo Waholanzi hawakuwa na njia ya kuleta upinzani wa dhahiri juu yetu.

Kwa kulishika jambo hili la kukaa mbali na mambo ya kitawala sasa jamia ya Ahmadiyya imesimamishwa karibu kila nchi na kila bara. Katika India na Afghanistan, na Ajemi na Iraq, na Sham na Kanaan pia. Hata jamia ya Ahmadiyya imesimamishwa katika Misri, Itali, Switzerland na Ujerumani pia. Jamia ya Ahmadiyya inapatikana katika Uingereza, Amerika, Malaya, Indonesia, katika Afrika ya Mashariki na ya Magharibi, Uhabeshi na Argentine. Kwa neno zima katika kila nchi jamaa kubwa au ndogo imekwisha kuwako. Na tena Waahmadiyya wanapatikana katika wenyeji hasa wa nchi hizo. Si kama ni Wahindi au Wapakistani tu walio Waahmadiyya huko, la. Na wako wenyeji wengine wenye utawa hasa waliojitupa maisha yao kwa ajili ya kufanya kazi ya dini ya Kiislam. Juzi juzi Luteli mmoja Mwingereza Bwana B.A. Orchard mejitoa maisha yake na sasa anafanya kazi ya ubashiri katika Uingereza. Anasali kwa mfululizo, hatumii kabisa ulevi, anafanya kazi kwa mkono wake, anachuma mali na katika mali ile anapiga chapa magazeti na anatoa hotuba za dini huko na huko. Sisi tunampa fedha kidogo, hata mfagiaji wa Uingereza anaweza kupata fedha zaidi kuliko tunazompa yeye. Vivyo hivyo Mdachi mmoja wa Ujerumani ameyatoa maisha yake wakfu kwa ajili ya kuutumikia Uislam, tena yeye ni ofisa wa jeshi la ulinzi, na baada ya taabu kubwa amepata cheti cha kufika Pakistan ili ajifunze elimu ya dini na amalize shauku ya moyo wake kwa kueneza dini ya Kiislam katika nchi zingine. Yuko Mjerumani mwingine aliye ni kijana, tena mtungaji wa vitabu, pamoja na mke wake ambaye pia ni mwana-chuoni, wanafikiria kutoa maisha yao, na hivi karibuni watafika Pakistan kujifunza elimu ya Kiislamu. Mtu mmoja wa Uholanzi amekwisha fungania atoe wakfu maisha yake na inatumainiwa ataambiwa kufanya kazi ya kubashiri Islam katika nchi nyingine. Hapana shaka idadi ya Waahmadiyya ni ndogo, lakini jambo linalotakiwa

kutazamwa ni hili ya kuwa kwa juhudi ya Jamia ya Ahmadiyya inasimamishwa Jamia ya Islam. Katika kila nchi watu wengi au wachache wanaingia katika jamia hii na hivyo wanaweka msingi wa umoja wa ulimwengu mzima. Watu wa kila firka wanaingia katika jamia hii. Mwanzo wa mwendeleo wa namna hii unakuwa mdogo, lakini baadaye unapata nguvu, na kwa kupanda mbegu ya umoja na itifaki wanashinda katika siku chache. Ni dhahiri ya kuwa kwa nguvu ya siasa ya kitawala, inakuwako haja gani kufanya jamia za kitawala lakini kwa nguvu ya dini na tabia nzuri, inakuwepo haja ya kutengeneza jamia ya kidini na tabia. Jamia ya Ahmadiyya inakaa mbali na mambo ya kitawala na siasa, kwa sababu isipate uvivu katika kazi yake ya kubashiri dini.

## **TARATIBU YA JAMIA YA AHMADIYYA**

Jambo la pili ni juu ya taratibu ya jamia ya Ahmadiyya. Ama kwa shauri la taratibu, ni jamia ya Ahmadiyya tu inayoweka mbele yake taratibu maalumu, na hakuna jamia nyingine iliyo na taratibu maalumu, na hakuna jamia nyingine iliyo na taratibu maalumu ya kazi yao. Jamia ya Ahmadiyya kwa kutazama na kupima shambulio la Ukristo, inashindana nao katika kila nchi. Katika zama hizi, bara iliyo nyonge kuliko dunia nzima au kwa sababu zingine, bara yenye nguvu zaidi kuliko bara zingine ni bara ya Afrika. Ukristo umeshambulia kwa nguvu zake zote juu ya Afrika. Na Wakristo wameanza kuonesha waziwazi nia yao; kwanza Mapadri tu walikuwa wanafikiri Afrika, baadaye *Conservative Party* ya Uingereza ikaiielekea kidogo, lakini sasa *Labour Party* ambayo inaishika Serikali ya Kiingereza pia imekwisha tangaza kwa kusema: Kuokoka kwa Ulaya kumo katika maendeleo ya Afrika. Lakini Ulaya ilikuwa inafahamu kuwa maendeleo haya ya Afrika na umoja wake unaweza kuifaa Ulaya kama wenyeji wake wote wawe Wakristo. Siri hii jamia ya Ahmadiyya ilikwisha jua miaka 24 mbele. Na kwa sababu hii miaka 24 kabla jamia Ahmadiyya ikawatuma Masheikh wake katika Bara hili na maelfu kwa maelfu ya Wakristo wakashika dini ya Kiislam kwa ubashiri wa Masheikh wa Kiahmadiyya. Kwa hivi sasa katika Afrika jamia ya Kiislam iliyo na taratibu bora kuliko jamia zingine ni jamia ya Ahmadiyya, ambayo kwa kushindana nayo Wakristo pia wakaanza kuona hofu. Na katika magazeti yao imesemwa mara

kwa mara ya kuwa juhudi ya jamia ya Waahmadiyya imeangusha bidiiya Mapadri wa Kikristo. Hii ndiyo hali ya Afrika ya Magharibi, juhudi ya jamia Ahmadiyya kwa kubashiri dini pia inaendelea katika Afrika Mashariki tangu miaka michache ijapokuwa kazi iko katika hali ya mwanzo na matukio si mazuri sana kama yalivyo katika Afrika ya Magharibi, lakini juu ya hayo Wakristo wameanza kukubali dini ya Kiislam, na inatumainiwa katika sehemu hii ya Afrika pia juhudi ya Masheikh wa Kiahmadiyya itaonesha matokeo mema, Insha Allah.

Katika Indonesia na Malaya pia jamia zimesimamishwa tangu miaka mingi, na kazi ya ubashiri wa Islam inafanywa, na Waislamu waliokuwa karibu kuacha dini ya Kiislam na walikuwa katika hali ya unyonge na ya kushindwa-shindwa, mbele ya Wakristo, jamia ya Ahmadiyya ikawapa nguvu, na kwa kuungana pamoja wakasimama imara mbele ya maadui.

Amerika ndiyo nguvu ya Ukristo iliyokwisha kuja mbele kuliko nguvu zingine za Ukristo. Hapo pia tangu miaka 24 Wabashiri wa Ahmadiyya wanafanya kazi. Na wenyeji maelfu na maelfu wamekwisha ingia katika jamia ya Ahmadiyya na kuwa Waislamu. Wanatoa rupia elfu na elfu kila mwaka kwa kazi ya kubashiri dini ya Islam huko. Kweli fedha hizi mbele ya mali ya Wakristo wa Amerika hazina kitu, na juhudi hii mbele ya juhudi za Mapadri haina maana, lakini juu ya hayo mashindano yameanzishwa na ufaulu tunapata sisi maana sisi tunapata watu katika wao na wao hawapati watu katika sisi. Basi kusemwa kwa nini Ahmadiyya imeanzisha jamia mpya haitakiwi bali inatakiwa kusema ya kuwa Ahmadiyya imesimamisha jamia moja hali haikuwapo jamia kabla yake. Je, jambo hili ni la lawama au la sifa?

## **SABABU YA KUKAA WAAHMADIYYA MBALI NA MATAIFA MENGINE.**

Baadhi ya watu wanasema mambo haya yaliyotajwa juu ni mema na yalitakiwa kuenezwa katika Waislamu wengine pia, lakini haikuwapo haja ya kusimamisha jamia nyingine. Majibu yake ya akili ni haya ya kuwa jemedari anaweza kuwatumia vitani watu wale tu waliokwisha andikwa katika jeshi. Wasioandikwa katika jeshi anawezaje kuwatumia? Isingeanzishwa jamia yoyote, mwanzilishaji wa jamia ya Ahmadiyya angepata wafanyakazi kutoka wapi na angemwamrisha nani? Na Makhalifa wake wangepata wafanyaji kazi wapi na wangewapa amri



nani? Au wangeanza kutembea sokoni na kumkamata kila Mwislamu na kumwambia pahali fulani leo iko haja ya Uislamu, wewe nenda huko na yeye angesema kujibu, mimi sikubali maneno yako. Baadaye aende mbele na akamate Mwislamu mwingine, na baadaye mtu mwingine, ingeweze kanaje kufanyika kazi? Ni jambo la akili ya kuwa ili kumaliza kazi ya taratibu maalumu lazima iwepo jamia maalumu. Na bila jamia ya namna hii haiwezekani kufanywa kazi yoyote maalumu na ya taratibu hasa. Kama isemwe: Jamia ingefanywa lakini wachanganyike na watu wengine pia; basi majibu yake ni: Kila mtu anawezaje kuwa tayari kufanya kazi inayoweza kumtia katika taabu kubwa na mashaka sana? Kazi ya namna hii wanaifanya wale wanaokuwa hawatazami chochote kingine katika dunia hii. Na watu wa namna hii wanatakiwa kuwekwa mbali na watu walioshughulika na mambo ya dunia. Kama hawa mahodari wa Kidunia watawafanya wale wanaofanya kazi za kidini bila kutazamia chochote wawe kama wao, basi nani atakayefanya kazi ya dini? Pia kukaa mbali na wengine kunaleta mastaajabu katika tabia za watu, na hivyo watu wanaanza kupeleleza wenyewe na na kufukua ukweli na mwisho siku moja wao pia wanakuwa windo la mwendeleo na taratibu ambayo walitaka kuivunja.

Basi upinzani huu wote ni matokeo ya kutofahamu na kufikiri sawasawa. Kama akili ishikwe, bila shaka inawezekana kufahamiwa ya kuwa kwa hakika njia ile hasa ni haki ambayo Uahmadiyya imeishika. Na kwa kufuata njia hii sawasawa inaweza kutengenezwa jamia ya watu watoao maisha yao sadaka kwa ajili ya kufanya kazi ya Islam. Na kama Uahmadiyya utaendelea kushika njia hii bila shaka idadi ya watu wa namna hii itaendelea kuwa zaidi hata batili na kufuru zitaona kuwa Islam sasa imeshika nguvu. Hapo kufuru na batili itashambulia Islam kwa nguvu zake zote lakini wakati huo utakuwa wakati wa shambulio umekwisha pita zamani. Ufaulu utakuwa kwa Islam na kufuru itashindwa. Sisi hatuwatili vizuizi njiani wale wanaofanya juhudi ya kiutawala na kisiasa. Sisi tunawaambia hao : Kama ninyi hamwezi kufahamu mambo yetu basi shauri yenu, endeleeni na mnayofanya. Lakini pia tunawataka wasituzuie katika njia yetu. Kama njia yao na mwendo wao waonekana kuwa mwema zaidi basi waungane nao. Na kama katika fikira za mtu mwendo wetu ni bora zaidi basi aungane nasi. Katika mwendo wao kujitolea sadaka ni kidogo lakini sifa ni kubwa, lakini katika mwendo wetu kujitoa sadaka kunatakiwa zaidi na sifa ni

kidogo. Wao wataendelea kupata sehemu yao na sisi tutandelea kupata sehemu yetu

Watu wanaofahamu kuwa kusimamisha Islam kwa hakika ya asili yake ni jambo la lazima zaidi wao watakuja na wataungana nasi. Na ambao wanataka na kupenda utawala na ufalme wa dhahiri wao watakwenda kwao na wataungana nao. Lakini kwa nini tupigane na tuhasimiane au tujadiliane? Wote wawili wanahangaika kwa sababu ya taabu ya umati wa Waislam iwapokuwa viungo ni mbalimbali. Wao wanasikia maumivu katika ubongo wao na sisi mioyo yetu ndiyo inapata taabu.

Mpaka hapa nimetoa majibu kwa namna ya akili. Sasa natoa majibu kwa namna ya kiroho na dini. Na mbele yangu namna ya kidini ndiyo hasaa namna inayoweza kushikwa.

## MAJIBU YA KIROHO

Majibu ya swali hili kwa namna ya kiroho na kidini ni haya ya kuwa ni desturi ya Mwenyezi Mungu tangu zamani, ufisadi unapoenea katika dunia, utakatifu na utawa unafutika kabisa. Watu wanaanza kuitanguliza dunia kuliko dini. Mungu humtuma

mtumishi Wake mmoja katika wakati huo kuwaongoza watu Wake na kuwarudisha na kuwapeleka watu Wake waliopotea kwenye njia Yake hasa na kuisimamisha duniani tena dini Yake. Wakati mwingine hawa wajumbe wanaotoka kwa Mwenyezi Mungu wanaleta sheria mpya, na pengine wanakuja kusimamisha sheria ya kwanza iliyofika zamani. Katika Qur`an Tukufu desturi hii ya Mwenyezi Mungu imekazaniwa sana. Na mara kwa mara wanadamu wameelekezwa kuifahamu rehema hii na ukarimu huu wa Mwenyezi Mungu anaounesha wakati wa uharibifu katika dunia.

Bila shaka Mwenyezi Mungu ana shani kubwa na mwanadamu mbele yeke ni hafifu hata kuliko mdudu, lakini hii pia ni haki ya kuwa kazi zote za Mwenyezi Mungu zimejaa hekima sana ya Yeye hafanyi kazi yoyote bila faida na bila sababu hasa. Mwenyezi Mungu anasema katika Qur`an Tukufu: *Wama khalaknassmawati wal ardha wama bainhuma laibina*, (Sura Dukhan); yaani hatukuviumba mbingu na ardhi bure, bali katika umbo lao Tumeweka haja, na haja ile ni ya kuwa mwanadamu

aoneshe sifa za Mwenyezi Mungu na awe maonesho Yake na hivyo amtambulisha Mwenyezi Mungu katika watu wasio na uwezo wa kuruka katika anga la kiroho. Tangu mwanzo wa dunia mpaka sasa, hivi ndivyo ilivyokuwa desturi ya Mwenyezi Mungu, Na katika nyakati mbalimbali Mwenyezi Mungu akawatuma wadhahirishaji mbalimbali wa sifa Zake katika dunia hii. Pengine sifa za Mwenyezi Mungu zimedhahirishwa na Adam a.s. na wakati mwingine na Nuhu, pengine zimedhahirika katika mwili wa Ibrahim, na zikang`aa katika mwili wa Musa. Daudi akaonesha Uso wa Mwenyezi Mungu katika dunia, na pengine Masihi akazagaza nuru ya Mwenyezi Mungu ulimwenguni. Mwisho wa wote, na kwa ukamilifu zaidi, Mtume Muhammad s.a.w. akazionesha sifazote za Mwenyezi Mungu kwa njia ya muhtasari na fasaha, kwa hali ya umoja na wingi, kwa shani na utukufu katika dunia hata manabii wote waliokuwa kabla yake wamezimika kama nyota mbele ya jua la utukufu wake. Baada ya Mtume s.a.w. sheria zote zimekwisha na njia za manabii waletao sheria zimefungwa. Si kwa sababu ya kupendelea bali kwa sababu Mtume Muhammad s.a.w. alileta sheria inayokusanya haja zote na inamaliza kusudi lote. Kitu kilichotakiwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu kimetimia,. lakini haikuwa dhamana kwa ajili ya watu wa Mungu ya kuwa wao hawataacha njia iliyonyoka, wala hawatasahau mafundisho yaliyo hai, bali Mwenyezi Mungu alisema katika Qur`an waziwazi: *Yudabbirul amra minassamai ilal ardhi thumma ya`ruju ilaihi fi yaumin kana mkdaruhu alfa sanatini mimma ta`uddun*. Yaani Mwenyezi Mungu atayasimamisha maneno Yake ya mwisho na sheria Yake ya mwisho kutoka mbinguni juu ya ardhi. Na upinzani wa watu hautakuwa kizuwizi katika njia Yake, lakini tena baada ya muda maneno haya yataanza kuruka kwenda mbinguni, na katika muda wa miaka elf moja yataondoka katika dunia.

Mtume s.a.w. anaweka muda wa kusimama dini mpaka miaka 300 kama ilivyoielezwa katika hadithi iliyoelezwa juu. Na katika Qur`an kwa neno la *Alif Lam Mim Ra* umeelezwa muda huu ni miaka 271 . Basi muda huu na muda ule wa miaka elf moja ya kupandishwa dini toka duniani mpaka juu uunganishwe, unakuwa muda wa miaka 1271. Kwa neno zima, muda wa kutoka roho ya dini katika dunia kwa mujibu wa Qur`an ni miaka 1271 au mwisho wa karne ya 13. Jinsi inavyojulikana katika Qur`an katika zama za namna hii Mwenyezi Mungu huleta kiongozi na mwoneshaji wa njia ya haki ili dunia isiingie katika mkono wa shetani

milele, na ufalme wa Mwenyezi Mungu usifutike kabisa katika dunia. katika zama hizi pia angekuja mtu mmoja kutoka kwa Mwenyezi Mungu haidhuru awe mtu gani, yeyote lakini lazima aje. Inawezekanaje; wafuasi wa Adam walipoharibika Mwenyezi Mungu akawatazama; wafuasi wa Ibrahim a.s. walipoingia katika ouvu Mwenyezi Mungu akawaangalia; wafuasi wa Nabii Musa a.s. walipopotea Mwenyezi Mungu akawaona; wafuasi a Nabii Isa waliposhikwa na upotevu ulio dhahiri Wenyezi Mungu akawatanabahisha; lakini wafuasi wa Seyidul Anbiya Mtume Muhammad s.a.w. waharibike, washikwe na upotevu na Mwenyezi Mungu akae kimya asiwatazame hali yao! Ulikuwako ubashiri kwa umati wa Muhammad .s.a.w. juu ya kuyaondoa maovu madogo madogo ya kwamba Mwenyezi Mungu atamtuma juu ya kila karne Mujaddid mmoja katika umati wake. Hayo hayo ndiyo aliyosema Mtume Muhammad s.a.w.: *Innallaha yab-athulihadhihil umati la ra'si ulli miati sanatini man yujaddidu laha dinaha* " yaani, hakika Mwenyezi Mungu ataleta mwanzo wa kila miaka mia mtu wa kuijadidisha dini (Abu Daud, jalada 2, uk. 241). Je, akili inaweza kukubali ya kuwa Mwenyezi Mungu amtume Mujaddid kila karne kwa kuyaondoa mambo madogo madogo. Lakini kwa fitina kubwa ambayo Mtume s.a.w. alisema: Tangu manabii wameanza kufika duniani wameetoa habari juu ya fitina hii, kiongozi yeyote asije na msuluhishi asifike, na mjumbe asitumwe, na isiinuke sauti ya kuwakusanya Waislamu juu ya dini ya haki kutoka kwa Mwenyezi Mungu na isiteremshwe kamba kutoka mbinguni ya kuwatoa Waislamu katika shimo la giza na upotevu? Mungu ambaye tangu mwanzo wa dunia, ameonesha huruma na rehema Yake, basi baada ya kumtuma Mtume Muhammad s.a.w. kwa hakika yakatokea machemko zaidi katika mto wa rehema Zake, wala haikufutika rehema Yake na ukarimu Wake . Kama Mwenyezi Mungu alikuwa zamani Mrehemevu basi sasa kwa ajili ya umati Muhammad .s.a.w. yeye anatakiwa kuwa mrehemevu zaidi kuliko zamani, Yeye alikuwa mkarimu zamani sasa, kwa ummati wa Muhammad s.a.w. Yeye anatakiwa kuwa mkarimu zaidi na bila shaka Yeye yu hivyo. Qur'an Tukufu na Hadithi za Mtume s.a.w ni shahidi ya kuwa utakapotokea uovu na upotevu katika umati Muhammad s.a.w. Mwenyezi Mungu atamtuma kiongozi na mjumbe kutoka Kwake, hasa katika siku hizi za mwisho, ambapo fitina ya dajjal itadhahirika na Ukristo utashinda, na Islam kwa hali ya dhahiri itashindwa, na Waislamu wataacha dini na

watahika mila na desturi za mataifa mengine. Hapo mfano kamili wa Mtume Muhammad s.a.w. atadhihiri na ataisuluhisha zama hii, ambayo Mtume Muhmaad s.a.w. amesema: "Hautabaki katika Uislam ila jina lake, wala haitabaki katika Qur'an ila maandiko yake." Roho ya Islam haitaonekana na maana ya Qur'an haitakuwa wazi.

Basi enyi wapenzi, kusimamishwa kwa Silsila ya Ahmadiyya kumekuwa kwa kufuata desturi hii ya zamani na sawa na ubashiri uliotolewa na Mtume s.a.w. na manabii wa kabla yake. Kama kuchaguliwa Seyyidna Ahmad a.s. hakukuwa vizuri kwa ajili ya kazi hii basi ni lawama juu ya Mwenyezi Mungu. Seyyidna Ahmad ana dhambi gani? Kama Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa ghaibu na hakuna siri yoyote iliyofichika Kwake, na kazi Zake zote zinakuwa na hekima nyingi basi ikumbukwe tena kuchaguliwa kwake Seyyidna Mirza Ghulam Ahmad kulikuwa sawa, na kumwamini yeye kuna heri kwa Waislamu na watu wengine wa dunia.

### **KAZI MAALUM YA SAYYIDNA AHMAD A.S.**

Seyyidna Ahmad a.s. hakuleta ujumbe mpya. Bali ujumbe ule ule ambao Mtume Muhmamad s.a.w aliwasikilizisha watu, lakini dunia ikasahau. Ujumbe ule ule ulioweka Qur'an duniani, lakini dunia ikageuza uso wake mbali nao. Na ujumbe ule ni huu: Mwumba wa ulimwengu wote ni Mwenyezi Mungu Mmoja. Yeye amemwumba mwanadamu kwa ajili ya mapenzi Yake na kwa kuungana naye. Na amemfanya yeye ili adhihirishe sifa Zake, kama alivyosema Mwenyezi Mungu

"Aliposema Mola wako kuwaambia malaika: Mimi nataka kumweka Khalifaa katika ardhi." Basi Adam na uzao wake ni Khalifa, yaani balozi wa Mwenyezi Mungu. Waameumbwa kwa ajili ya kuzidhihirisha sifa za Mwenyezi Mungu. Hivyo imelazimishwa kwa kila mwanadamu afanye maisha yake sawa na sifa za Mwenyezi Mungu. Na kama balozi, katika kazi zake zote, aelekee mara kwa mara kwa bwana wake. Na mtumishi kabla ya kuinua hatua yake anatazama kwa Mola wake, hivyo ni wajibu kwa mwanadamu aungane na Mwenyezi Mungu kwa kadri ambayo Mwenyezi Mungu amwongoze kila wakati na katika kila kazi naye awe mpenzi kuliko vitu vyote. . Na katika mambo yote awe

katika hali ya kumtegemea Yeye. Na kwa kuwamalizia wajibu huu Seyyidna Hadhrat Mirza GhulammAhmad, Masih Aliyehadiwa a.s. amefika duniani. Ilikuwa kazi yake kuwafanya watu wa dunia kuwa watu wa dini na kuusimamisha utawala wa Kiislam mioyoni mwao, na kumkalisha Mtume s.a.w katika kiti chake cha enzi ya kiroho ambacho ili kumtoa kwenye kiti hicho nguvu za shetani kwa siri na kwa dhahiri zinashambulia.

Kwa kumaliza wajibu huu Seyyidna Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. amefanya kazi hii kwanza kuliko kazi zote zingine ya kuwa amewaelekeza Waislam kwenye roho na ubongo wa dini na kuwafahamisha washike ganda lake tu. Na akawahimiza ya kuwa dhahiri ya amri pia ni jambo kubwa, tena lazima, lakini bila kushika undani na roho ya mafundisho mtu hawezi kuendelea mbele na kupata ustawi. Kwahiyo Seyyidna Ahamad akaanzisha jamia, na katika agano la baiat akaweka sharti ya kukiri kuwa: "MIMI NITATANGULIZA DINI JUU YA DUNIA.'

Kwa hakika huu ulikuwa ndiyo ugonjwa - kutanguliza dunia juu ya dini na kuhangaika kwa ajili ya dunia tu - uliokuwa unawangamiza Waislam; ingawa dunia ilikuwa imekwisha toka mikononi mwao juu ya hayo walikuwa wanaikimbilia. Mwendeleo wa Islam mbele yao ulikuwa kupata utawala wa kidunia. Na maana ya ustawi wa Uislam ilikuwa katika fikira zao kuendelea kwao katika biashara na mafunzo, hali Mtume Muhammad s.a.w. hakufika ili watu waitwe Waislamu, bali alikuja kwa kuwafanya watu wawe Waislam sawasawa ambao sifa yao inaelezwa na Qur'an hivi: *Man aslama wajhahu lillah* - Ajitupaye kabisa mwili wake na roho yake kwa Mwenyezi Mungu na aweke haja zake zote za kidunia chini ya haja zake za kidini . Ijapokuwa jambo hili linaonekana jambo dogo, lakini kwa hakika hii ndiyo tofauti kati ya dini ya Kiislam na dini zingine. Islam haisemi msijifunze elimu, wala haisemi msifanye biashara wala haisemi msifanye kazi za sanaa wala haisemi msifanye bidii kuimarisha serikali zenu, bali dini ya Kiislam inayabadilisha mawazo ya mwanadamu tu juu ya mambo haya. Katika dunia kazi zote zinakuwa na mawazo ya namna mbili, ya kwanza: katika ganda kupata kiini na ya pili katika kiini kupata ganda. Mtu anayetamani kupata kiini katika ganda si lazima ashinde katika makusudio yake, bali mara nyingi yeye anashindwa. Lakini mtu anayepata kiini hupata na ganda pia. Mtume s.a.w na wafuasi wake ilikuwa juhudi yao yote kwa ajili ya dini lakini

hawakunyang`anywa katika neema ya kidunia pia. Ni jambo la kuwaida watu watakaopata dini dunia itawakimbilia kama mjakazi, lakini si lazima kwa kupatikana dunia dini ipatikane katika ganda si lazima ashinde katika makusudio yake, bali mara nyingi yeye anashindwa. Lakini mtu anayepata kiini hupata na ganda pia. Mtume s.a.w. na wafuasi wake ilikuwa juhudi yao yote kwa ajili ya dini, lakini hawakunyang`anywa katika neema ya kidunia pia. Ni jambo la kawaida watu watakaopata dini dunia itawakimbilia kama mjakazi. Lakini si lazima kwa kupatikana dunia dini pia ipatikane. Mara nyingi katika hali ya namna hii dini haipatikani, hata pengine dini iliyokuwa kidogo mioyoni mwao inatoka pia. Seydna Ahmad a.s. kwa kufuata mwendo wa manabii kwa amri ya Mwenyezi Mungu akahimiza dini. Alipokuja Waislamu walikuwa na mwendeleo wa namna mbili: mmoja ulikuwa wamekwisha anguka na kuwa dhaifu na wanyonge na hivyo wakahimizwa wafanye bidii kupata nguvu ya kidunia. Mwendeleo wa pili akaanzisha Seyyidna Ahmad a.s. kuwa wanatakiwa wafanye bidii kujielekeza kwenye dini, na katika matokeo yake dunia pia bila shaka itapatikana kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

## **MABADILIKO YALIYOTOKEA**

Baadhi ya watu wamekosa walipofahamu kuwa Mwendeleo wa Seyyidna Ahmad a.s. ni sawa na mwendeleo wa watu wa tarika za muridi. Kwa dhahiri wao wanahimiza sala na saumu, lakini wanawakalisha watu wazima wenye afya faraghani na kuwafanya kama wanawake wenye kutawa. Kama Seyyidna Ahmad a.s. angefanya hivyo bila shaka angewahimiza watu kupata ganda kwa jina la kiini. Lakini yeye hakufanya hivyo. Jinsi yeye aliovyotia mkazo juu ya amri za kidini ndivyo alivyotia mkazo kuwa dini inatoka kwa Mwenyezi Mungu kwa kuzitia nuru akili za mwanadamu na kutia mwanga katika ubongo wake na kuzinoa fahamu zake. Yeye akasema: Mtu anayefuata dini kwa kweli wala hashiki udanganyifu, dini huleta tabia nzuri katika dhati ya mtu huyo. Dini hutia nguvu ya kutenda matendo, na dini inamtia moyo wa kutoa sadaka na kujinyima mwenyewe kwa kuwapendelea wengine. Yeye akasema: Shikeni dini, salini, fungeni saumu, fanyeni hija, toeni Zaka. lakini salini zile sala zilizosemwa na Qur`an, na fungeni

zile saumu zilizooneshwa na Qur`an na toeni zaka iliyotajwa katika Qur`aan. Qur`an haiwatakieni kukaa na kusimama, wala haiwatakieni mkae katika njaa. Wala haiwatakieni mwache nchi yenu bila sababu, wala haiwaambieni kupoteza mali zenu. Qura`an Tukufu inasema juu ya sala: *Innasalata tanhaa anilfahshaai walmunkar*, -Sala inawachisheni mambo maovu na yachukizayo. Basi kama hayatokei matokeo ya sala yaliyosemwa katika Qur`an, sala yenu si sala. Juu ya saumu Qur`an inasema: *La`allakum tattakuna* - Saumu imelazimishwa ili mpate utawa na tabia nzuri. Lakini kama ninyi mnafunga saumu na hampati matokeo haya basi ni dhahiri nia yenu si sawa, na ninyi hamfungi saumu, ila mnajiweka katika njaa na Mungu hawatakieni mkae katika njaa. Kwa hija Mwenyezi Mungu amesema: Inazuia mawazo ya uasi na inayaondoa mambo yanayoleta majadiliano kati ya jamia. Basi hija ni kwa ajili ya kuondoa ufasiki na ugomvi. Kwa ajili ya Zaka amesema: *Khudh min amwaalihim asakatan tutahhiruhum wa tazakkiihim bihaa* - Chukua katika mali zao sadaka ukiwafanya safi na kuwatakasa. Zaka imelazimishwa kwa kumtakasa mtu na jamia, na kwa kusafisha moyo na fikira. Basi kama matokeo hayo yasitokee, haji yenu na zaka zenu ni ya ria tu. Basi salini, fungeni saumu, fanyeni hija, toeni zaka, lakini nitawakubalieni kama sala zenu ni sala, au saumu zenu au hija zenu au zaka zenu kuwa kweli za haki kama matokeo yao yaonekane yaani mjepushe katika maovu, na utawa upatikane ndani yenu, na mkae mbali kabisa na ubishi, ufasiki na ugomvi; mpate usafi wa moyo na fikira, na watu watakasike. Lakini mtu asiyekuwa na matokeo ya namna hii mimi sitamfahamu kuwa ni mmoja wa jamia yangu, maana yeye ameshika ganda wala hakushika kiini kilicho hasa makusudio ya Mwenyezi Mungu. Hivyo Seyyidna Ahmad a.s. akawahimiza watu katika ibada zote kwa kukitafuta na kukipata kiini na akasema: Hakuna amri yoyote ya Islam isiyokuwa na hekima. Mwenyezi Mungu haonekani kwa macho, bali anaonekana kwa moyo. Mwenyezi Mungu haguswi na mkono, bali anaguswa na mapenzi. Makusudio ya dini si kuvitawala macho na mikono, bali inapovitawala macho na mikono inavitawala kwa kuusafisha moyo na fikira, ili mwanadamu apate nguvu ambazo zimwezeshe kumwonesha Mwenyezi Mungu na kumgusa na apate nguvu ambazo zimwezeshe kusikia sauti ya Mwenyezi Mungu. Kwa neno zima Seyyidna Ahmad a.s. kwa kuyahimiza mambo ya namna hii amefungua njia mpya ya maendeleo na ustawi wa dini ya Kiislam, na



katika matokeo yake ikadhihirika jamia moja, na jamia hii imetanguliza dini juu ya dunia na ikaanza kwa mwendeleo wa Islam na kwa kusimamisha utawala wa kiroho wa Mtume Muhammad s.a.w ikaanza kutoa sadaka na juhudi ya kila namna. Fikirini jamia ndogo ya Waahmadiyya na upande mwingine taifa kubwa la Waislam. Je, jinsi jamia Ahmadiyya inavyoshughulika kwa kueneza dini ya Kiislam na kuiendesha mbele, Waislamu wengine walio ni mara elfu nyingi zaidi kuliko wao wanafanya kazi hata nusu au robo ya kazi ya Waahmadiyya? Mabadiliko haya yametokea kwa namna gani? Kwa sababu Seyyidna Ahmad a.s. aliwahimiza Waahmadiyya watangulize dini juu ya dunia. Lilipodhihirika jambo hili kwa Waahmadiyya vitendo vyao vikabadilika kwa sura mpya. Sala ya Ahmadiyya mkweli haiwezi kuwa sawa na sala ya Mwislamu mwingine. Sura ni ile ile, maneno ni yale yale, lakini kiini ni kingine. Ahmadiyya anasali kwa ajili ya sala, na anasali kwa kuzidisha maungano yake pamoja na Mwenyezi Mungu. Huenda mtu aseme: je, watu wengine hawasali kwa kuzidisha maungano yake pamoja na Mwenyezi Mungu? Ninajibu: La. Kama mtafikiri mtajua ya kuwa kwa bahati mbaya Waislamu wameanza kufikiri ya kuwa haiwezekani mtu kupata bi nafsi yake kuungana na Mwenyezi Mungu. Makosa makubwa yameenea katika Waislamu ya kuwa Mwenyezi Mungu hasemi na watu Wake leo. Wala watu hawawezi kumfanya Mwenyezi Mungu akubali maombi yao. Zaidi ya miaka mia moja imepita Waislamu wamekataa kushuka kwa wahyi wa Mwenyezi Mungu. Bila shaka walikuwapo watu kabla ya muda huu katika Waislamu waliokuwa wanakubali wahyi wa Mwenyezi Mungu unashuka. Siyo kukubali tu bali pia walikuwa wanadai ya kwamba Mwenyezi Mungu anazungumza nao. Lakini tangu muda wa miaka 100 msiba huu uliwashukia Waislamu na wakawa wakataaji kabisa wa kushuka kwa wahyi wa Mwenyezi Mungu. Hata baadhi ya wanazuoni wakasema ya kuwa kulisema jambo hili pia ni kufuru. Seyyidna Ahmad a.s. aliyekuwa Masihi Aliyehidiwa a.s. akadai: "Mwenyezi Mungu anazungumza nami. Siyo mimi tu bali pia atazungumza na yule atakayenifuata mimi na kushika mwendo wangu na, na kukubali mafundisho yangu, na atapokea mwongozo wangu." Yeye akaweka mbele ya watu wa dunia maneno ya Mwenyezi Mungu kwa mfululizo aliyoyapata Kwake. Na akawahimiza wafuasi wake pia wafanye bidii kuzipata neema hizi za Mwenyezi Mungu. Akasema "Mwislamu anaomba mara tano kwa Mwenyezi Mungu maombi haya:

*Ihdinassiratal mstakima siratalladhina anamta alaihim, Ee Mungu utuoneshe njia iliyo sawasawa, njia ya wale uliowaneemesha, yaani Manabii wa zamani. Basi ingewezekanaje maombi yake haya kuharibika na kupotea milele na Mwenyezi Mungu asimfungulie Mwislamu yeyote yaliyofunguliwa kwa Manabii wa zamani? Na asizungumze na Mwislamu yeyote alivyokuwa anazungumza na Manabii wa zamani?*

Hivyo Seyidna Ahmad a.s. akakiondoa kabisa kifuniko kilichokuwa kimefunika mioyo ya Waislamu. Mimi sisemi kila Ahmadiyya, lakini nasema kuwa Ahmadiyya yeyote aliyefahamu sawasawa makusudio ya Seyyidna Ahmad a.s. hasali kwa kumaliza wajibu tu bali anasali kana kwamba anakwenda kwa Mwenyezi Mungu kupata chochote na amekwenda kwa Mwenyezi Mungu ili apate maungano mapya naye., basi mtu anayesali kwa nia ya namna hii ni wazi kuwa sala yake haiwezi kuwa sawa na sala za watu wengine. Seyyidna Ahmad a.s. ametia mkazo juu ya kuungana na Mwenyezi Mungu kwa kadiri ambayo akasema: "Mwenyezi Mungu ametoa dalili nyingi kwa kuhakikisha madai yangu. Lakini siwambieni ya kuwa fikirini dalili hizi. Kama ninyi hampati nafasi ya kufikiria dalili hizi na kuzitambua au hamwoni haja au mnafanamu kuwa akili zenu zitakosa kukata hukumu katika mambo haya. Basi nawaelekezeni *kuwa mumwombe Mwenyezi Mungu kwa ajili yangu, mtake mwongozo Kwake. Kama huyu ni mkweli Ee, Mola wetu utujulishe. Na kama yu mwongo, utuweke mbali naye.*" Na akasema : "Kama mtu yeyote ataomba kwa uhalisi wa moyo na bila uwadui wowote, siku chache, bila shaka Mwenyezi Mungu atamfungulia njia ya mwongozo, na atamdhihirishia ukweli wangu." Wako watu mamia na mamia na maelfu na maelfu waliofanya bidii sawa na njia hii na wakapata nuru kwa Mwenyezi Mungu. Angalieni dalili hii iliyo nyeupe! Mwanadamu anaweza kukosa katika akili yake lakini Mwenyezi Mungu hawezi kukosa katika kuongoza kwake. Ana yakini ya namna gani juu ya ukweli wake huyu mtu ambaye kwa kutambua ukweli wake anaweka mbele za watu njia za namna hii za kukata hukumu! Je, mtu mwongo anaweza kusema, nendeni kwa Mwenyezi Mungu na mumwulize habari zangu? Je, mtu mwongo anaweza kufikiri ya kuwa hukumu itakatwa kwa kupewa haki mimi? Mtu asiyetoka kwa Mwenyezi Mungu bali anawaambia watu washike njia ya kukata hukumu kama ilivyoenezwa juu bila shaka mwenyewe anakata hukumu juu ya nafsi yake na anakata miguu yake kwa shoka lake mwenyewe. Lakini Seyyidna Ahmad a.s. kila mara na siku zote

ameweka mbele ya watu njia hii: "Nina dalili za ukweli wangu elfu na elfu, lakini kama ninyi hampati utulivu katika dalili hizo basi msisikie maneno yangu wala msisikie ya maadui, bali nendeni kwa Mwenyezi Mungu na mwulize Kwake, je, mimi ni mkweli au mwongo? Kama Mwenyezi Mungu aseme: Mimi ni mwongo, bila shaka tena mimi ni mwongo. Lakini kama Mwenyezi Mungu aseme mimi ni mkweli basi tena ninyi mna udhuru gani wa kukataa ukweli wangu?"

Enyi wapenzi, tazameni, njia hii jinsi ilivyo sawa na ya haki kabisa kwa kukataa hukumu. Maelfu na maelfu wakapata faida kwa kushika njia hii, na watu wote ambao watakubali kushika njia hii ya kupata hukumu iliyo sawa wanaweza kupata faida. Katika njia hii ya kukataa hukumu ilikuwamo hekima kubwa ya kuwa Seyyidna Ahmad a.s. alikuwa anafahamu kwamba dini ni mbele kuliko dunia. Yeye alikuwa anasema, "Mwenyezi Mungu alitoa macho ili tuvitazame vitu vya kidunia, na akatupa akili ili tuvifahamu vitu hivyo. Na kwa kuvifanya vitu vya kidunia vionekane akaumba jua Lake na akaziumba nyota pia. Basi ingewezekanaje Mwenyezi Mungu aliyefanya hivyo kwa ajili ya mambo ya kidunia asingetengeneza njia ya kuonesha mwongozo wa kiroho? Bila shaka mtu yeyote anapotaka kuviona vitu vya kiroho Mwenyezi Mungu humfungulia njia. Yeye Mwenyewe amesema katika Qur'an: *"Alladhinajahadu fina alaanadhiyannahum subulana,"* yaani, watu ambao kwa kuonana nasi wanafanya juhudi bila shaka tunawaonesha njia Zetu.

Kwa kifupi Seyyidna Ahmad .a.s. Mjumbe aliyeahidiwa, ameifungua njia ya kutanguliza dini juu ya dunia kwa ajili ya wafuasi wake na pia akaiweka njia mbele ya watu wanaomkataa. Mola wetu ni mmoja aliye hai., Yeye ndiye anayeendesha taratibu ya ulimwengu hata sasa - taratibu ya ulimwengu wa dunia na dini. Ni lazima kwa mwaminio apate mwungano zaidi na zaidi kwa Mwenyezi Mungu, na aendelee kufika karibu Yake. Na mtu ambaye hakudhihirika kwake mwongozo ni lazima kwake pia atake nuru ya mwongozo kwa Mwenyezi Mungu, na kwa msaada Wake afanye bidii afike kwenye haki. Basi kazi hasa na ujumbe hasa wa Seyyidna Ahmad a.s. ilikuwa kuwasuluhisha watu na kuwapeleka wanadamu kwa Mwenyezi Mungu. Na watu ambao walikwisha kata tamaa ya kuonana na Mwenyezi Mungu watie yakini katika mioyo yao na tamaa ya kuonana na kuwajulisha watu maisha ambayo waliyapata watu waliokuwa katika siku za Nabii Musa a.s. na Isa a.s. na Manabii wengine.

## CHEM-CHEM YA MAARIFA

Enyi! wapenzi tazameni, baada ya kuvisoma vitabu vya zamani, tena tazameni habari za wazee wenu (wa Kiislamu) wa zamani, je, maisha yao yalikuwa maisha ya kidunia tu? Je, kazi zao zilikuwa zinafanywa kwa hila za kidunia tu. La, Bali wao walikuwa wanahangaika usiku na mchana ili kupata mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Na katika hawa waliopata ufaulu wakipata sehemu kubwa katika miujiza na ishara za Mwenyezi Mungu. Na hii ndiyo iliyokuwa maisha iliyowapambanua katika watu wengine. Lakini leo jambo gani linalowapambanua Waislamu katika Mabaniani na Wakristo na mataifa mengine? Kama hawana jambo la namna hii, basi iko haja gani ya Islam? Lakini hakika ni hii, liko jambo linaloweza kuwapambanua Waislamu lakini Waislamu wamelisahau. Na jambo lile ni hili ya kuwa katika dini ya Kiislam maneno ya Mwenyezi Mungu na wahy Wake vinaendelea. Na daima inawezekana mtu bi nafsi yake kuungana na Mwenyezi Mungu. Hii ndiyo maana ya mafuriko ya chemchem ya maarifa ya Mtume Muhammad s.a.w. Siyo maana ya mafuriko ya maarifa yake kama tushinde katika mitihani ya vyuo vikubwa na tuwe M.A. au B.A. Je Mkristo hawi B.A. na M.A.? Wala si maana ya mafuriko ya maarifa yake ya kuwa tumeendesha banda kubwa la sanaa. Je, Mkristo au Baniani au Singasinga haendeshi banda la manma hii? Wala si maana ya maarifa yake kama sisi tumefungua jumba kubwa la biashara na tumeanzisha kazi ya biashara zetu katika nchi mbalimbali, maana hii pia Wakristo na Mabaniani na Mayahudi wote wanafanya. Basi maana hasa ya mafuriko ya maarifa ya Mtume Muhammad s.a.w. ni hii ya kuwa kwa kumfuata yeye mwanadamu apate bi nafsi yake maungano pamoja na Mwenyezi Mungu na moyo wake uanze kumwona Mwenyezi Mungu, na roho yake iungane naye na asikie maneno Yake matamu na zidhihirike ishara mpya za Mwenyezi Mungu kwa ajili yake. Hilo ndilo lisilopatikana kwa mtu yeyote katika dunia isipokuwa kwa kuingia katika utumwa wa Mtume Muhammad s.a.w. na kwa jambo hilo tu wafuasi wa Mtume Muhammad s.a.w. wamepambanuka katika mataifa mengine. Kwenye jambo hili Seyyidna Ahmad a.s.akawaelekeza Waislamu na jambo hilo akaliweka mbele ya watu wasiomkubali yeye kuwa, kama asemavyo: "Mwenyezi Mungu amenipa lulu iliyokuwa imepotea zamani. Na zawadi iliyoharibika Mungu ameirudisha kwangu na haya yote nimepata kwa baraka za Mtume Muhammad s.a.w. na

kwa kumfuata yeye. Na baraka zake zimenifikisha mpaka cheo hiki.

Ziko kazi nyingine nyingi alizozifanya Seyyidna Ahmad a.s. lakini zote ni chini ya kazi hii kubwa na mfano wao ni kama matawi ingawa kazi hizo pia ni zenye adhama na za shani. Lakini kazi hasa ilikuwa kuwahimiza watu watangulize dini juu ya dunia na mambo ya kiroho juu ya mambo ya kiwiliwili. Na bila shaka dini ya Kiislam itashinda dini zingine zote kwa njia hii. Naam tutazilinda nchi zetu kwa bunduki na mizinga na pia tutawashinda maadu zetu kwa kuzitumia silaha hizi. lakini ushindi wa Islam juu ya dunia nzima hautapatikana ila kwa kuishika njia ile ya kiroho ambayo Seyyidna Ahmad a.s. amehimiza ishikwe. Mwislamu atakuwa Mwislamu hasa atakapoanza kutanguliza dini juu ya dunia, atakapoanza kupendelea vitu vya kimbingu juu ya vitu vya kidunia, ndipo maisha yale ya kifidhuli ya dunia yanayoendelea katika nchi zetu kwa sababu ya mataifa ya Ulaya yatafutika yenyewe. Na mwanadamu si kwa sababu ya kuambiwa na mtu mwingine bali mwenyewe kwa nafsi yake ataziacha fidhuli hizi na ataingia katika maisha yenye maana na ulimi wake utapata nguvu itakayotia athari katika roho za watu. Na jirani zake wataughulika kujipaka rangi zake; na Wakristo na Mabaniani na watu wa dini zingine wataanza kusema jinsi walivyosema watu wa Makka: Laiti wangekuwa Waislamu! Na pole pole kauli yao hii, sawa na watu wa Makka, itabadilika katika matendo na wao watakuwa Waislamu, namna mtu yeyote hawezi kukaa mbali na maneno mazuri. Kwanza inakuwa shauku, baadaye inakuwa tamaa, halafu yanatokea mavuto na mwisho mwanadamu anafika kwenye jambo hilo. Hivyo ndivyo itakavyotokea sasa pia. Kwanza Islam itaingia sawasawa katika mioyo ya Waislamu, kisha alama yake itaonekana juu ya miili yao, baadaye watu wasiyo Islamu watakuwa tayari kuushika mwendo wa hawa Waislamu walio kamilika, na dunia itajaa Waislamu, na Islamu itaonekana kila pahali.

## NJIA ZA USHINDI

Enyi wapenzi, katika makala hii fupi siwezi kueleza dalili kwa maelezo mengi wala siwezi kuweka mbele yenu mambo yote ya ujumbe wa Uahmadiyya kwa fasaha, lakini nimeweka mbele yenu haja ya Uahmadiyya na makusudio yake. Nawaombeni mfikirie sana maneno haya na mfahamu ya kuwa mwendeleo wa kidini hauwezi kushinda duniani kwa njia za kidunia tu. Mwendeleo wa kidini siku zote unapata ustawi na kushinda kwa kujitakasa nafsi kwa ubashiri na kwa sadaka. Tangu siku za Nabii Adam a.s. mpaka sasa ambalo halikutokea, sasa pia halitatoka. Na namna ulivyoendelea kuenea ujumbe wa Mwenyezi Mungu duniani kwa kuzishika njia zile hasa, pia ujumbe wa Mtume Muhammad s.a.w. utaenea katika dunia. Basi kwa kujirehemu nafsi zenu, na kuwahurumia za watoto wenu na jamaa zenu, na kuwarehemu watu wa makabila yenu na kwa kuihurumia nchi zenu, fanyeni bidii kusikia maneno ya Mwenyezi Mungu na ujumbe Wake na kuufahamu ili ifunguliwe milango ya rehema za Mwenyezi Mungu kwa ajili yenu, na Mwendeleo wa Islam usiakhirishwe. Bado kazi nyingi tunazozotakiwa kizifanya, na sisi tunawangojeeni kwa ajili ya kazi hizo. Maana ustawi na ufaulu unaotoka kwa Mwenyezi Mungu pamoja na miujiza vinaugana pia kwa kueneza dini. Karibuni na bebeni mzigo huu pamoja na sisi ambao kuubeba kumelazimika kwa ajili ya mwendeleo wa Islam na ufaulu wake. Kweli ni lazima kuitazama sadaka na mtu kujinyima nafsi yake kwa ajili ya wengine, na lawama na adhabu pia ni lazima vyote fikirawe katika njia hii. Lakini katika njia ya Mwenyezi Mungu kifo ndicho kinachotoa maisha hasa, na bila kushika kifo hicho Islam haiwezi kushinda. Fanyeni hima na kikombe hiki cha mauti mkiweke mdomoni ili kwa mauti yenu na mauti yetu Islam ipate maisha na uhai, na dini ya Mtume Muhammad s.a.w. tena iinuke na kustawi, na kwa kuikubali mauti hii sisi pia tupate starehe ya maisha ya milele katika ulinzi wa mpenzi wetu Allhumma Amin.

MIRZA MAHMUD AHMAD,

Khalifa pili wa Seyyidna Ahmad a.s.

**Hakika ya Ahmadiyya**  
**(Message Of Ahmadiyyat)**  
**By Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmood**  
**Ahmad r.a. Khalifatul masih II**  
**(Swahili translation).**

This book was first published as a lecture delivered by Khalifatul Masih II r.a. on 31st October 1948 at Sialkot Pakistan and appeared in Al Fazl newspaper in Urdu language.

Due to its importance in establishing the true picture and removing all doubts about the message of Ahmadiyyat, it was translated into Swahili language by Maulana Sheikh Mubarak Ahmad.

The book covers shortly but precisely about:  
The Beliefs of Ahmadiyyat in different controversial matters.  
The need of establishing new Jamaat.  
Systems of Jamaat Ahmadiyya in Preaching Islam and  
Changes which have already occurred as the effect of the teachings of Ahmadiyyat.

**Ahmadiyya Muslim Jamaat**  
**Tanzania.**